# UCHUNGUZI WA REJESTA YA MAZUNGUMZO YA ASKARI POLISI KATIKA LUGHA YA KISWAHILI JIJINI MBEYA

**KIBOPILE KISSA**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YAKUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YAUZAMILI (M.AKISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma tasinifu hii iitwayo: ***Uchunguzi wa Rejesta ya Mazungumzo ya Askari Polisi Katika Lugha ya Kiswahili Jijini Mbeya, na*** kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya (M. A. Kiswahili - Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

………………………………………

Dkt Hanna J. Simpassa

(Msimamizi)

………………………………………

Tarehe

**HAKIMILIKI**

Hairuhusiw ikuiga au kunakili kwa namna yoyote sehemu yoyote ile ya tasinifu hii kwa njia yoyote kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria chaTanzania kwa niaba.

# TAMKO

Mimi**, Kissa Kibopile,** nathibitisha kuwa tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au nyingine yoyote.

………………………………

Saini

………………………………

Tarehe

# TABARUKU

Kazihii ninaitabaruku kwa Baba yangu mzazi marehemu Dkt John Burton Kibopile kwa ajili ya chachu aliyoipanda kwangu ya kunijengea misingi ya kusoma kwa bidii.

## SHUKURANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kufikia hatua hiiya kukamilisha utafiti wangu nilioufanya kwa miaka kadhaa. Yeye ndiye aliyenijaalia nguvu,uwezo, fikra na utashi wa kufanya utafiti huu ambao leo hii nauhitimisha. Shukurani za pekee ziende kwa msimamizi wangu Dkt. Hanna Simpasa, kwa kutumia muda wake, kwa hali na mali katika kunitia moyo nilipoonekana kukata tamaa. Licha ya mapungufu niliyokuwa nayo aliweza kunivumilia, akaipitia kazi yangu, akaisahihisha na kunielekeza vilivyo ili kuhakikisha kuwa inakuwa inavyotakiwa kuwa.

Ninakishukuru Chuo Kikuu Huria cha Tanzania hasa Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii wakiwemo walimu wangu Dkt. Zelda Elisifa (Mkuu wa Idara ya Sanaa na Sayansi ya jamii), Dkt. Omar Mohamed, Dkt. Hadija Jilala, Dkt. Nestory Ligembe, Jonas Buhori na Isaya Sigalla. kwa taaluma, maarifa na ushauri walionipa pia kwa ushirikiano mzuri ulioniwezesha kukamilisha kazi hii. Nasema asante sana, Mungu awajaalie mema.

Vilevile shukrani za pekee ziwafikie baba yangu Kanali mstaafu Nsa Kaisi, mama yangu mpendwa Suma Kibopile, Mjomba Burton Mwasomola - mkurugenzi wa TAMISEMI, Dkt. Patrick Kibopile, Dkt. Lute Kibopile, Paulina Kibopile - afisa utumishi wa jiji, Mhandisi Magesa Mwita kwa kujitoa kwao kwa hali na mali kuhakikisha ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili inatimia. Bila kuwasahau watumishi wa Mungu Joshua Chris, Emmanuel Msangi, Boniface Mwamposa na wote waliokuwa wakiniombea katika kipindi chote, Mungu awabariki sana. Aidha nawashukuru wanafunzi wenzangu hasa Hamisa Nalinga na wengine wote, nikiwa

kama kiongozi wa wanafunzi wa shahada ya uzamili ya Kiswahili wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa mwaka 2016/2018, kwa ushirikiano mkubwa tuliokuwa nao Mungu awajalie mafanikio mema.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia rejesta katika mazungumzo ya askari polisi katika vituo vya kazi jijini Mbeya.Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu: mosi, kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi inavyozungumzwa, pili kueleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi, tatu kujadili sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi. Utafiti umefanyika katika jiji la Mbeya. Data za utafiti huu zilipatikana kwa mbinu za ushuhudiaji, hojaji na dodoso. Mtafiti alitumia sampuli ya watu 30 wakiwemo askari polisi na askari wa usalama barabarani. Kutoka uwandani tulipata jumla ya maneno ishirini (20) yaliyokusanywa kisha kuchanganuliwa ili kubaini rejesta katika mazungumzo ya askari polisi katika vituo vya kazi. Kutokana na ushuhudiaji pamoja na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa zipo rejesta zinazotumika katika jeshi la polisi ambazo zimeundwa kwa kufupisha tungo. Kwa mfano neno Lindo na afande ni miongoni mwa maneno ya rejesta yaliyotokana na kufupisha tungo katika jeshi la polisi nayo hutumika mara nyingi zaidi katika mazungumzo ya askari polisi. Pia neno mlalamikaji, mtuhumiwa na mshtakiwa hutumiwa katika rekodi za askari polisi. Katika lengo la pili la utafiti huu, askari polisi walikuwa na maoni yafuatayo: Kutokana na takwimu za utafiti zilionyesha kuwa watoa habari walithibitisha kuwa kazi kubwa ya rejesta yao ni kuficha usiri. Katika lengo la tatu, matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa sababu kubwa ya ukuaji wa rejesta ni kuwepo kwa watumiaji na matukio mbalimbali ya kulinda raia na mali zao. Utawala wa jeshi la polisi uendelee kufanya utafiti na kuibua rejesta zingine zaidi ili kuboresha utendaji kazi.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** .......... ii

**HAKIMILIKI** .......... iii

**TAMKO** .......... iv

**TABARUKU** .......... v

**SHUKURANI** .......... vi

**IKISIRI** .......... viii

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... xiii

**KIAMBATANISHO** .......... xiv

**ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO** .......... xv

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**UTANGULIZI** .......... 1

1.1 Utanguliziwa Jumla .......... 1

1.1.1 Usuli wa Utafiti .......... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .......... 3

1.3 Malengo ya Utafiti .......... 3

1.3.1 Malengo ya Jumla .......... 3

1.3.2 Malengo Mahususi .......... 4

1.3.2 Maswali ya Utafiti .......... 4

1.4 Umuhimu wa Utafiti .......... 4

1.7 Mipaka ya Utafiti .......... 5

1.8 Hitimisho .......... 5

**SURA YA PILI** .......... **6**

**MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA** .......... **6**

2.1 Utangulizi .......... 6

2.1.1 Dhana ya Rejesta .......... 6

2.2 Mapitio ya Maandiko .......... 7

2.3 Pengo la Utafiti .......... 18

2.4 Kiunzi cha Kinadharia .......... 18

2.5 Hitimisho .......... 20

**SURA YA TATU** .......... **21**

**MBINU ZA UTAFITI** .......... **21**

3.1 Utangulizi .......... 21

3.2 Eneo la Utafiti .......... 21

3.3 Populesheni, Sampuli na Usampulishaji .......... 22

3.3.1 Populesheni .......... 22

3.3.2 Sampuli .......... 22

3.3.3 Usampulishaji .......... 23

3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data .......... 24

3.4.1 Ushuhudiaji .......... 24

3.4.2 Dodoso .......... 25

3.4.3 Mahojiano/Usaili .......... 26

3.5 Vifaa vya Utafiti .......... 27

3.5.1 Simu ya Mkononi .......... 28

3.5.2 Shajara na Kalamu .......... 28

3.5.3 Kompyuta .......... 28

3.6 Uchambuzi wa Data ........ 29

3.7 Changamoto za Ukusanyaji wa Data ........ 29

3.8 Hitimisho ........ 29

**SURA YA NNE ........ 30**

**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA ........ 30**

4.1 Utangulizi ........ 30

4.2 Watoa Habari ........ 31

4.3 Kiwango cha Rejesta Matumizi ya Rejesta Askari Polisi ........ 31

4.3.1 Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi ........ 31

4.3.2 Kiwango na Matumiziya Rejesta ya Askari Polisi Wa Usalama Barabarani Zinavyozungumzwa ........ 35

4.4 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi ........ 40

4.4.1 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi ........ 40

4.4.2 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari wa Usalama Barabarani ........ 43

4.5 Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi ........ 46

4.5.1 Maelezo kuhusu Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi ........ 46

4.5.2 Mjadala wa Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari wa Usalama Barabarani ........ 48

**SURA YA TANO ........ 50**

**MATOKEO YA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 50**

5.1 Utangulizi ........ 50

5.2 Muhtasari wa Utafiti ........ 50

5.3 Mapendekezo ........ 53

5.4 Mapendekezo Kwa Tafiti Fuatishi ........ 53

5.5 Hitimisho........................................................................................................53

**MAREJEO........................................................................................................54**

**KIAMBATANISHO ..............................................................................................58**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Idadi ya Watafitiwa Katika Vituo .......... 22

Jedwali 4.1: Msamiati Uliopatikana Toka Kwa Askari Polisi na Askari wa Usalama Barabarani .......... 30

Jedwali 4.2: Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta za Askari Polisi .......... 31

Jedwali 4.3: Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi .......... 32

Jedwali 4.4: Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi .......... 33

Jedwali 4.5: Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi .......... 34

Jedwali 4.6: Data zaidi Zionyeshazo Kiwango cha Matumizi ya Rejesta za Askari Polisi wa Usalama Barabarani .......... 36

Jedwali 4.7: Data zaidi za Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani .......... 37

Jedwali 4.8: Kiwango na matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani .......... 38

Jedwali 4.9: Data zaidi za Kiwango na matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani .......... 39

Jedwali 4.10: Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi .......... 41

Jedwali 4.11: Data zaidi Kuhusu Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari wa Usalama Barabarani .......... 43

Jedwali 4.12: Data zaidi za Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi .......... 46

Jedwali 4.13: Data zaidi za Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari wa Usalama Barabarani .......... 48

**KIAMBATANISHO**

Kiambatanisho A: Dodoso la Utafiti Kuhusu Rejesta Katika Vituo vya Kazi vya Askari Poilisi Jijini Mbeya ........................................................... 58

Kiambatanisho B: Msamiati Uliokusanywa ................................................................ 62

## ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO

( )Maelezo au ufafanuzi kuhusu jambo fulani

“ ” Unukuziwa maelezo au maneno yaliyosemwa na mtu

**TUKI** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

**TATAKI** Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

**_**...................Kutenganisha jina / Kutenganisha miaka

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utanguliziwa Jumla

Utafiti huu unahusu mtindo wa lugha (unaojulikana kama rejesta) ambao unatumika katika vituo vya kazi vya askari polisi jijini Mbeya.Lengo la kwanza ni kubainisha namna rejesta ya askari polisi inavyozungumzwa. Lengo la pili ni kueleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi. Lengo la tatu ni kubainisha sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi. Sura hii ya utangulizi imegawanywa katika sehemu kuu nane. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi wa sura hii, sehemu ya pili inaeleza usuli wa tatizo la utafiti, sehemu ya tatu inafafanua kiini cha tatizo la utafiti, sehemu nne inataja malengo ya utafiti, sehemu ya tano inaweka bayana maswali muhimu ya utafiti, sehemu ya sita inatoa maelezo kuhusu umuhimu wa utafiti huu, sehemu ya saba inafafanua mawanda ya utafiti na sehemu ya nane inatoa hitimisho la utafiti.

### 1.1.1 Usuli wa Utafiti

Lugha ni chombo kinachounganisha watu katika jamii, watu hutambua kikundi chao cha kijamii kutegemea aina ya lugha wanayotumia**,** kwa maana ya kwamba matumizi ya lugha kwa njia fulani ndio huwafungamanisha watu wa kikundi fulani na kuwatambulisha. Askari polisi kama kikundi cha kijamii nao wana lugha yao ambayo huwatambulisha wao kama kikundi maalumu. Askari polisi nikiungomuhimu katika kulinda usalama wa raia na mali zao. Katika kutekeleza majukumu yao hayo askari polisi wameteua mtindo wa lugha (rejesta) ili kukidhi mahitaji yao.

Mgullu (1999) akimnukuu Trudgil (1990) anasema kuwa “lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa kwa mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake”. Kutokana na fasili hiyo tunaona kuwa lugha ni chombo ambacho hutumiwa na jamii au makundi fulani ya jamii kwa ajili ya mawasiliano, utamaduni wa jamii au kundi fulani la watu wana namna yao ya mawasiliano ili kukidhi mahitaji yao. Mahitaji hayo hupelekea kuwa na mtindo tofauti wa mawasiliano, mitindo hiyo ndio hupelekea kuwepo kwa rejesta mbalimbali.

Todd (1987) amefasili lugha ni mfumo wa ishara ambazo kwazo watu wanawasiliana. Kamusi ya isimu ya lugha (1990) lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Mekacha (2000) anadai kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu na ishara za kisarufi ambazo kwazo watu wa jamii fulani ya jugha huwasiliana na kupokezana utamaduni wao. Massamba na wenzake (1999) wataalamu wengi wa isimu ya lugha wanaelekeana kusema kwamba lugha ni sauti za nasibu ambazo hutumiwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao.

Kwa ujumla, lugha ni mfumo wa sauti, ishara, nasibu zilizokubaliwa na jamii fulani yenye utamaduni sawa kwa madhumuni ya kuwasiliana, kuelewana na kushirikiana katika upashanaji habari. Halliday (1989) anafasili rejesta Kama mtindo wa lugha kutegemeana na kazi au shughuli maalumu. Kwa fasili hii tunaona kuwa kila mazingira au shughuli inayohusisha kundi moja la jamii fulani huwa na rejesta tofauti na kundi jingine. Aidha Habwe na Karanja (2010) wanasema kuwa ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano makundi ya kijamii huibua mitindo na istilahi zao zinazowawezesha kurejea shughuli za kundi husika. askari polisi kama kikundi cha

kijamii pia wanamtindo wao wa mawasiliano ambao huwawezesha kutimiza mahitaji yao.

Utafiti huu unahusu mtindo wa rejesta unaozungumzwa na wafanyakazi wa vitengo mbalimbali vya jeshi la polisi katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya. Katika kufikia lengo la utafiti huu tulijikita katika kuchunguza matumizi ya rejesta yanavyojitokeza katika mawasiliano ya askari polisi wa vitengo mbalimbali katika Jiji la Mbeya. Pia tulieleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi. Vilevile tulibainisha sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Lugha ni chombo kinachotumika kwa mawasiliano baina ya jamii moja na nyingine. Lugha ikitumiwa vizuri hujenga mahusiano mazuri lakini ikitumika vibaya huweza kuleta utengano. Watu hutambua kikundi chao cha kijamii kulingana na lugha wanayoitumia. Askari polisi pia kama kundi la kijamii wanaweza kuwa na rejesta yao. Hivyo, utafiti huu unachunguza rejesta ya mazungumzo ya Askari polisi katika lugha ya Kiswahili katika jiji la Mbeya.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya jumla na malengo mahususi. Malengo hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

### 1.3.1 Malengo ya Jumla

Utafiti huu unachunguza rejesta katika mazungumzo ya askari polisi katika vituo vya kazi mjini Mbeya.

### 1.3.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahususi matatu:

(i) Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi inavyozungumzwa.

(ii) Kueleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi.

(iii) Kujadili sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi.

### 1.3.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulikusudiwa kujibu maswali matatu:

(i) Je, ni kwa kiwango gani rejesta ya askari polisi huzungumzwa?

(ii) Je, nini kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi wa Jiji la Mbeya?

(iii) Je, ni sababu zipi zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi?

## 1.4 Umuhimu wa Utafiti

Kijamii utafiti huu utasaidia kutambua uwepo wa lugha inayotumiwa na kuwabainisha askari polisi kama kundi jamii. Kwa wasio wamilisi wa lugha ya kiswahili utafiti huu utawasaidia kujua rejesta inayotumika katika vituo vya askari polisi jijini Mbeya. Hivyo wao wenyewe wataweza kuhusisha aina hii ya rejesta na rejesta zingine katika lugha ya Kiswahili. Kitaaluma utafiti huu una manufaa yafuatayo:

Utachangia kupanua maarifa yaliyopo na yasiyokuwepo kuhusu mtindo wa lugha unaojulikana kama rejesta, pia utachangia kuongeza maarifa mapya katika isimu jamii ya kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatachochea watafiti wengine kutaka kuchunguza mtindo wa rejesta za makundi malimbali ya kijamii na lugha nyingine za kibantu na kusaidia kubaini uhusiano au tofauti za kimuundo baina ya lugha hizo. Vilevile

matokeo ya utafiti huu ni msaada katika kuwaeleimisha wanafunzi wa somo la kiswahili hususani Isimujamii hasa kuhusu utambulisho wa kijamii

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita kuchunguza mtindo wa lugha ujulikanao kama rejestakatika vituo vya kazi vya askari polisi, kipengele pekee kilichochunguzwa ni kubaini kiwango cha rejesta ya askari inavyozungumzwa, kazi ya rejesta na sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta hiyo.

## 1.8 Hitimisho

Sura hii imebeba mwongozo wa sura zinazofuata kwa kutoa utangulizi na kubainisha mambo yaliyofanyiwa utafiti ikiwemo tatizo la utafiti, malengo, maswali na umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti na shughuli zilizofanywa ili kupata data za kujibia maswali. Sura inayofuata inahusu mapitio ya maandiko pamoja na nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imehusisha mapitio mbalimbali ya maandiko pamoja na tafiti tangulizi zilizochunguza au kuandika juu ya rejesta katika lugha. Aidha, imebainisha pengo lililoachwa na tafiti zilizotangulia. Pia imeeleza na kufafanua kiunzi cha kinadharia ambacho kimeongoza utafiti huu.

### 2.1.1 Dhana ya Rejesta

Rejesta ni istilahi ya kisinonimia kwani inarejelewa kwa istilahi tofautitofauti na waandishi tofautitofauti kama 'mtindo, sajala, sajili na rejista' (King'ei, 2010). Mekacha (2011), Labov na Trudgill (1966), wanatumia istilahi 'rejesta'. Lackie- Tarry (1995), Halliday, (1978), Giles na Coupland (1991) wanatumia istilahi 'mtindo wa lugha' 'utumizi/matumizi ya lugha' na lugha ya….." kwa mfano, lugha ya kanisani, lugha ya kisheria na kadhalika. Kwa upande wao Mwansoko (1991) naMwangomango (keshatajwa) wanatumia istilahi 'mtindo wa lugha'. Licha ya kuwa na istilahi tofafauti bado zote zinamaanisha lugha inayotumika katika muktadha fulani kwa madhumuni maalumu. Katika kazi hii ilitumika istilahi 'rejesta ya……' kwa kiasi kikubwa, palipokuwa na ulazima wa kutumia istilahi zingine ili kujenga uelewa wa jambo lililozumgumzwa, istillah 'mtindo wa lugha ya…' zilitumika. Kuna rejesta za maandiko na za mazungumzo. Katika maandiko rejesta huonekana katika matini, kwa mfano, katika maandiko rejesta huonekana katika matini, kwa mfano, katika vitabu, magazeti, mabango ya matangazo na kadhalika. Katika mazungumzo, rejesta hujitokeza, kwa mfano katika mazungumzo ya watu, sokoni, kanisani, mahakamani na

kadhalika. Kwa ujumla zipo rejesta za aina nyingi kwa sababu ya shughuli mbalimbali za kila siku za watu. Mwangomango (katajwa) anasema kuwa mtindo ni aina za mwachiko wa lugha kulingana na mazungumzo na matumizi yanayotokeleza jambo mahususi. Mtindo ya lugha yoyote inaweza kuwa mingi mno hata ikawa vigumu kutoa idadi kamili kwa kuwa shughuli za watu pia ni nyingi.

## 2.2 Mapitio ya Maandiko

Sehemu hii imewasilisha mawazo makuu yatokanayo na mapitio ya maandiko mbalimbali yahusuyo rejesta. Sababu za kupitia maandiko mbalimbali ni kutokana na ukweli kwamba, utafiti unaofanyika hujengwa katika msingi wa utafiti uliotangulia na kwamba maandiko yaliyotangulia kuhusu lugha itumikayo kulingana na muktadha yanasaidia kujua nini kimefanywa na nini hakijafanywa na watafiti waliotangulia. Rejesta ni kipengele cha lugha ambacho kimeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali wa isimu. Katika ‘wikipedia, *the free encyclopedia’* inaeelezwa kuwa kwa mara ya kwanza dhana ya rejesta ilitumiwa na mwanaisimu Thomas Bertram Reid (1956) na mnamo miaka ya 1960 kundi kubwa la wanaisimu kama Halliday na Hasan (1976), Trudgill (1983) na Biber (1988) likaona ipo haja ya kutofautisha lugha inayotokana na mtumiaji yaani lahaja (ingawa si lengo la utafiti huu.

Kuzungumzia lahaja) na lugha kulingana na matumizi, kwa maana ya lugha inayotumika katika muktadha maalumu yaaani rejesta. Kutokana na maneno hayo inaonekana wazi kuwa wanaisimu wa miaka ya nyuma, yaani kabla ya 1960, walishindwa kutofautisha dhana ya lahaja na ile ya rejesta. Kwao lahaja na rejesta vilionekana kuwa kitu kilekile, yaani mtindo wa lugha. Lakini baaada ya miaka ya 1960 baadhi ya wanaisimu waligundua kuwa kuna tofauti kati ya lahaja na rejesta na

hivyo dhana hizo mbili ilibidi zitenganishwe. Kazi hii ilishughulikia dhana ya rejesta pekee. Maaandiko mengi yaliyopitiwa katika kazi hii yalionekena kutumia lugha ya…', 'mtindo' na rejesta kuliko istilahi zingine. Utafiti huu pia ulitumia istilahi 'rejesta' Kwa kiasi kikubwa na penye ulazima wa kutumia istilahi nyingine ili kusaidia kazi hii kueleweka vizuri, zilitumika istilahi za 'lugha ya.' au 'mtindo wa lugha'.

King'ei (2010) anatumia istilahi nne ambazo ni mtindo, sajala, sajili na rejesta. Istilahi hizi zimetumika katika mkururo mmoja kama zinavyoonekana na zote zikiwa na dhana ileile ya mtindo wa lugha unaotumika katika muktadha maalumu. Aidha, King'ei (keshatajwa) anadai kwamba somo la mtindo limetanda na kugubika isimu na pia vipengele vya fasihi. Anaendelea kusema kuwa wataalamu tofauti wamejaribu kufafanua maana ya mtindo kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, Cryastal na Davy (1969) wanafafanua mtindo kuwa ni mazoea ya mtu binafsi ya kuzungumza au kuandika. Yaani, njia za matumizi ya lugha huwa ni za kibinafsi na huweza kumtambulisha mtumiaji wa lugha kwa kiasi au kiwango fulani. Mtindo pia unaweza kuelezwa kama njia au tabia kwa kiasi au kiwango fulani. Mtindo fulani pia unaweza kuelezwa kama njia au tabia ya matumizi ya lugha miongoni mwa watu wa jamii – lugha fulani kwa kipindi maalumu katika historia. Kwa mfano, kuna mtindo wa ushairi wa zamani (kabda ya karne 19), Kiingereza cha kabda ya kristo, karne za kati, cha kisasa na kadhalika.

Vilevile mtindo hutumika kueleza uwanja mzima wa ubora wa matumizi ya lugha ya kiusomi kwa kuitofautishana lugha ya kimazungumzo au lugha ya kawaida.

Anaendelea kusema kuwa hata hivyo, neno ‘mtindo’ hapa linatumika kwa maana ya ‘mtindo au sifa zinazoambatana na matumizi ya lugha katika taalamu fulani’.

King’ei (katajwa) anaeleza zaidi kwamba matumizi ya lugha katika mazingira ya taalumu hujulikana kama rejesta, sajili au sajili au sajali. Mifano ya sajili ya mazungumzo na sajili ya vyombo vya habari. Kwa mfano, katika vichwa vya habari huwa vinaandikwa namna itakayovuta macho na kufikirisha.

Kwa mfano, ‘**Saba Kizimbani’.** Kichwa hicho cha habari kina maana kuwa ‘**watu saba wafikishwa kizimbani**’ na wala SABA si jina la mtu na wala SABA KIZIMBANI si nomino zinazomtaja au kumbainisha mtu aitwaye Saba Kizimbani. Lakini kiundani kichwa hicho cha habari ni usemi unaojitosheleza na ni sawa kabisa katika muktadha huo wa habari kwa sababu matumizi yoyote ya lugha huzingatia muktadha inamotumika lugha hiyo. Hivyo zipo sababu zinazofanya matumizi ya lugha yawe kama yalivyo. Kwa mfano, katika habari lugha itakiwayo ni lile iliyofupishwa lakini yenye kueleweka kwani vinginevyo maneno mengi huchukua nafasi kubwa na habari zingine hukosa sehemu za kuandikwa na hivyo kusababisha hasara katika gazeti kwani kazi ya gazeti aghalabu iko kibiashara zaidi. Pia anazielezea sajili nyingine kama sajili za michezo, sheria, sayansi, biashara, mazungumzo ya simu, siasa, hotelini, mahakamani, hospitalini, kituo cha poilsi, shuleni, mapenzi, vijana wa kisasa, na sajili ya ofisini.

Kwa mfano: ***Mkuu wa kazi: Juma kwa nini jana hukufika kazini?***

***Mhudumu: Samahani mkuu, mimi jana sikufika kazini kwa sababu nilikuwa naumwa.***

Chanzo: Msanjila na Wenzake (2011:7)

Kwa upande mwingine mfanyakazi huyuhuyu aliulizwa na mfanyakazi mwenzake anayefanya naye kazi ofisi moja swali lielile aliloulizwa na mkuu wake wa kazi. Lakini kwa mfanyakazi mwenzake lugha aliyotumia ilikuwa taofauti kama ifuatavyo:

***Mfanyakazi: Juma, kwa nini jana hukufika kazini?***

***Mhudumu: Aisee we acha tu, jana mwenzako nilikuwa kitandani hoi,*** *basi* ***nikaamua moja***

Chanzo: Msanjila na Wenzake (2011:7)

Vifungu hivyo vyenye italiki vinaonyesha kuwa muktadha tofauti wa mazungumzo baina ya wahusika ndio uliomshawishi mhudumu azungumze namna hizo tofautitofauti kwa wahusika tofauti lakini kwa mada ileile ya kumtaka aeleze sababu za kutofika kazini jana. Namna hiyo ya mhudumu kujieleza tofauti kwa mkuu wake wa kazi na kwa mfanyakazi mwenzake lakini kwa lengo lile lile la kusema sababu za kutafika kazini jana, huitwa rejesta. Hali hiyo ya kawaida na ndiyo inayotawala maisha yetu ya kila siku kwa sababu kila kitu kinapaswa kuthaminiwa namna kilivyo na hali hiyo ndiyo husababisha matumizi mbalimbali ya lugha.

Pia, Mbunda (1992) anaeleza rejesta kuwa ni jinsi, mtindo, ama namna mbalimbali ya mamlaka ya matumizi ya lugha. Kwa mfano, kuna tofauti ya msingi kati ya lugha ya kuandika na lugha ya kuzungumza. Mtu anavyoandika ni tofauti na jinsi anavyozungumza. Hii pia ni aina ya rejesta. Aidha, anasema kuwa kwa upande mwingine, kuna rejesta zinazotokana na umri. Kwa, mfano, vijana wana rejesta yao, wazee wana yao, wanawake wana yao na kadhalika. Marafiki nao wana rejesta yao. Rejesta zingine zinazotajwa ni rejesta za mitaani, mazungumzo ya kisheria, maelezo ya kisiasa yaliyoandikwa kitaaluma, uandishi wa kifasihi na kadhalika. Pia, kuna

rejesta za hotelini. Kwa mfano, hapo Mbunda (katajwa) anadai kuwa lugha katika migahawa na hotelini zina utaratibu wake ambao katika hali ya kawaida inaweza isieleweke. Kwa mfano:

***A: Nani kuku?***

***B: Mimi.***

***A: Wapi chai moja?***

***C: Nipe chai moja tafadhali.***

Chanzo:

Katika mazungumzo hayo **A** kwa mfano anapouliza: ***Nani kuku?*** Ana maana kuwa nani angependa kula (nyama ya kuku). Hana maana ya kumwainisha mtu aitwaye **kuku**. Au ***chaimojawapi***? Ana maana ya nani anahitaji kikombe kimoja cha **chai**. Katika hali halisi hakuna chai moja wala chai mbili kwani chai hazihesabiki bali vinavyohesabika ni vikombe vya chai. Sababu zinazofanya matumizi ya lugha yawe kama yalivyo yawezekana ni kutaka kurahisisha mazungumzo kutokana na kuwa na idadi kubwa ya wateja ambao wote wanahitaji kuhudumiwa muda huohuo mmoja. Hii ni rejesta ya hotelini ambayo ni lazima itumike hivyo katika mazingira na kutaka kurahisisha huduma kwa wateja na pia kuiletea hoteli faida.

Nao Labov na Trudgill (1966) walifanya utafiti katika jamii na kuona namna konsonanti ***[r]*** inavyosikika miongoni mwa matabaka manne ambayo ni tabaka la chini, la kati na tabaka la juu, katika maneno kama***'guard', 'bare'***, na ***'beer'*** matokeo yalionyesha kuwa, usikikaji wa konsonanti ***[r]*** ulitofautiana miongoni mwa matabaka hayo. Vilevile viwango vya matumizi ya msikiko wa ***[r]*** mwanzoni au mwishoni mwa sauti vilitofautiana kulingana na viwango vya madaraja ya watu na matabaka yao.

Katika tabaka la chini konsonanti **[r]** ilisikika kwa wazi na kwa nguvu kabisa kama konsonanti awali. Katika tabaka la chini juu ***[r]*** ilisikika Kwa nguvu kidogo lakini si kama katika tabaka la chini. Katika tabaka la kati juu ***[r]*** ilisikika Kama konsonanti mwanzoni mwa sauti ya neno pasipo uwazi sana kiasi cha msikilizaji kushindwa kubainisha vizuri. Katika tabaka la juu sauti ***[r]*** haikusikika kabisa kwani imemezwa ndani ya neno. Kwa majumuisho, utafiti ulibaini kuwa utamkaji wa sauti ***[r]*** ni wa kimsikiko na wenye nguvu zaidi katika tabaka la chini na hakukuwa na msikiko katika tabaka la juu.

Aidha Labov (1966) aliteua makundi mbalimbali ya wazungumzaji wenye umri tofauti na kazi tofauti kama vile wavuvi, wanawake na vijana. Utafiti uligundua kwamba vijana wenye umri kati ya miaka (31 - 45) walikwepa matumizi ya lugha sanifu ya New England. Pia matumizi ya maneno kama ***'walkin'*** na ***' talkin'*** ambayo yapo kwenye mfumo usio sanifu yalitumika badala ya ***'walking'*** na ***'talking'***. Labov aligundua kuwa vijana walitumia lugha ya namna hiyo kwa sababu walitaka kujibainisha kuwa wao ni kundi fulani kijinsia na kitabaka.

Kwa upande wa wavuvi Labov (keshatajwa) aligundua kuwa katika uzungumzaji wao walitia chumvi nyingi, walipiga chuku za kutosha na maneno yao kwa ujumla yalijaa vionjo mbalimbali. Ilionekana kuwa wakati mwingine watu hubatizana majina kama***ngasa, perege, papa*** na kadhalika. Hii ni kwa sababu ya kazi waifanyayo ambapo mtu hupewa jina kulingana na tabia yake inayolingana na aina hiyo ya samaki. Vilevile ugunduzi mwingine ulionyesha kuwa, vijana na wazungumzaji walio katika mfumo wa elimu.

Aidha Biber (1988) anaiona rejesta kuwa ni msingi muhimu au sababisho la utofauti wa kilahaja katika jamii. Wazo la Biber (keshatajwa) linaungwa mkono na kress (1993) ambaye anaiona rejesta kuwa ni jumla ya matumizi yote ya lugha yanayohusiana na muktadha maalumu. Aidha, Kress (keshatajwa) anaainisha rejesta mbalimbali kama vile lahaja, tarafa, masimulizi, hotuba, mtindo, tanzu, msuko wa matukio na sifa bainifu. Anaendelea kusema kuwa lugha huweza kutumika kwa mitindo mbalimbali kwa kadiri ya uhitaji wa mtumiaji. Kwa mfano, uandishi mbalimbali wa kitaalamu na usio wa kitaalamu kama vile wa makala, hotuba, insha hadithi na barua, hizo zote ni rejesta tofautitofauti.

Hivyo, kwa kutafsiri maelezo ya Kress (kashatajwa) rejesta ni jumla ya mambo mengi katika matumizi ya lugha. Hapa Kress (katajwa) anaitazama lahaja kuwa ni aina ya rejesta, mtazamo ambao ulitumiwa na wanaisimu wa nyuma, kabda ya miaka 1960 na baadaye ukakosolewa na kurekebishwa na wanaisimu waliofuata baada ya ya miaka ya 1960, akiwemo Kress mwenyewe kuwa rejesta ni lugha inayotokana na matumizi ya lahaja ni lugha inayotokana na mtumiaji. Msimamo huu wa Kress (kashatajwa) wa kuitaja tena lahaja kama ni aina mojawapo ya rejesta ni kujichanganya mwenyewe. Kwa mtazamo wa mtafiti wa kazi hii lahaja si aina ya rejesta bali ni kipengele cha lugha kinachojitosheleza chenyewe.

Leckie - Tarry (kashatajwa) anaeleza kuwa rejesta ni mjengo wa kinadharia unaohusiana na namna matini ilivyojengwa kulingana na muktadha unaoizunguka, pia kulingana na mfumo wa lugha na mfumo wa kijamii uliopo. Tafsiri ya maelezo hayo ya Leckie- Tarry (keshatajwa) ni kwamba, dhana ya rejesta inaweza kutazamwa pia

kisemantiki. Aidha anaweka wazi kuwa sifa za kisemantiki za matini zina tabirika kwenye muktadha. Kwa mtazamo wake maana ya neno hutokana na muktadha lilimotumika.

Hymes (1972:46) anaeleza namna ya kuchunguza na kufafanua matumizi ya lugha anasema kuwa “tunachunguza matumizi ya lugha kwa kuzingatia ni nani anatumia lugha ipi, anatumia na nani, wapi na katika muktadha upi?

Vilevile gazeti la Sani toleo la 28 uk 14, limezungumzia rejesta ya kijiweni, iliyoshirikisha kundi la vijana wa rika moja, mazungumzo yao yalikuwa hivi;

“Big!  Tumesikia ***unamisi skuli*** siku hizi ni kwa nini?”

“Ah, si Yule ***ticha*** Sululu…….Eti kunipakazia ***nimechapa*** madaftari ya shule” (kimya)

“***Maticha*** wote wakapanga wanishike ili ***wanibiti,*** lakini niliwatoka mfano wa ***roketi”***

(kimya lakini wana nyuso za mshangao)

***_chekini washikaji, dingi*** angeniona si ingekuwa hatari, hatari”……

Nalo gazeti la mfanyakazi machi, (1988) liliandika rejesta ya kijiweni, mazungumzo yalikuwa hivi; Yee! Mjumbe, degree kama degree mimi oyee tu, nadhani “***umeiget fresh”*** kuhusu nguvu – nguvukazi au vipi? Mimi “***longtime”*** niko hapa “***town”*** bila “***job nadunda na mishemishe”*** tu. Na vilevile ndio nina wiki ee tu tangu “***niopoe*** hiki ***kiwapa***…”

Vilevile Halliday na Hassan (1976) wanaona kuwa kuna mambo matatu yanayoukilia uteuzi wa rejesta fulani ambayo ni mada ya mazungumzo, uhusiano baina ya

wahusika na njia ya mawasiliano kwa mfano njia ya mdomo au njia ya maandishi. Maelezo hayo pia yanaungwa mkono na Giles na Coupland (1991) na Trudgill (1983:101) wao wanasema kwamba wazungumzaji huteua kutumia mtindo fulani wa lugha kukidhi mahitaji yao ya kijamii kwa wakati huo. Hivyo, uwezo wa kiakili wa mzungumzaji wa lugha wa kuweza kuhaulisha malengo ya kijamii ndiyo yanayomshawishi kuchagua aina ipi ya mtindo wa lugha aitumie.

Baker (1992) anaeleza kwamba lugha ina muktadha wake wa matumizi. Anaeleza kuwa sajili za lugha zitiliwe maanani kwa kutambua sifa za matumizi lugha kwa kutegemea muktadha unaohusika.

Mwansoko (1991) anafafanua kuwa kutokana na hali ya ukaribiano baina ya watu si ajabu kuliona kundi la watu kama vile maprofesa, madaktari, makarani, wahudumu wa ofisi na kadhalika likiongea kwa namna fulani kwa sababu linaunganushwa na lugha iliyo wazi kwa wote katika mazingira yao ya kazi. Mfano mwingine anaoutoa ni wa wasafiri katika basi ambapo hutokea mazungumzo yanayowasisimua na kuwachekesha watu wote bila kujali matabaka yao. ***Kwa mfano; 'mzigo si dhamana yetu, wenzetu wamo kazini, tafadhali chungamzigo wako'***. Hapa ina maana kuwa kila abiria atunze mzigo wake asifikiri kwa kuwa yumo ndani ya basi wenye gari ndio wanapaswa kumlindia mali yake. Pia, wanatahadharishwa wawe makini na mali zao kwani kuna watu ndani ya basi ambao si waaminifu.

Michira (1993) alifanya utafiti wa uchambuzi wa matini katika lugha ya wachuuzi wa soko la Gikomba na lugha ya matangazo ya biashara redioni nchini Kenya kwa kutumia mtazamo wa kimtindo, aligundua kuwa kazi zote mbili zilionyesha

kuchanganya msimbo sintaksia ya lugha zote mbili ile ya matangazo na ya wachuuzi ni nyepesi na kulikuwa na makosa mengi ya kisarufi.

Aidha, Leckie - Tarry (1995) anaeleza kuwa kutokana na muainisho wa kutosha wa ishara zinazotokana na muktadha inawezekana kutabiri sifa za kisemantiki za matini. Anafafanua zaidi kwamba kinadharia rejesta rejesta huhusiana na muktadha, na kwa hiyo miktadha haukwepeki. Vilevile Lackie - Tarry (katajwa) anaeleza kuwa maana zote katika mawasiliano hupatikana kutokana na muktadha. Kwa hiyo ni muhimu kubainisha, kuainisha na kufafanua muktadha ambao ndio elementi muhimu katika kupambanua rejesta. Leckie - Tarry (kashatajwa) anaeleza kuwa rejesta ni mjengo wa kinadharia unaohusiana na namna matini ilivyojengwa kulingana na muktadha unaoizunguka, pia kulingana na mfumo wa lugha na mfumo wa kijamii uliopo. Tafsiri ya maelezo hayo ya Leckie - Tarry (keshatajwa) ni kwamba, dhana ya rejesta inaweza kutazamwa pia kisemantiki. Aidha anaweka wazi kuwa sifa za kisemantiki za matini zina tabirika kwenye muktadha. Kwa mtazamo wake maana ya neno hutokana na muktadha lilimotumika.

Cruse (2004) anaeleza kuwa maana ya neno huweza kutafsiriwa tofautitofauti kulingana na muktadha husika. Anatoa mfano wa neno ***"menu"*** na kusema kuwa mteja akiwa hotelini akisema ***"tafadhali naomba menu"*** ataletewa karatasi au fomu yenye orodha ya chakula na bei zake.

Naye Mekacha (2011) anasema kuwa rejesta hutokana na wasemaji wake kufanya kazi tofauti. Hapa Mekecha (keshatajwa) ana maana kuwa matumizi ya lugha huwa tofauti katika kazi tofauti, kwani kila shughuli hutumia lugha yake ambayo huwa

tofauti na lugha ya shughuli nyingine. Mekacha (keshatajwa) anaendelea kuelezakuwa ni jukumu letu kujua matumizi tofautitofauti ya lugha ya kiswahili. Mathalani, msemaji wa kiswahili anaweza kusalimia kwa kusema **“Habari za leo?** au ‘ **Ah! Vipimambo?** Au ‘**shikamoo”;** na anayesalimiwa anaweza kujibu kwa namna tofauti kwa salamu ileile. Salamu anayotoa anayesalimia na jibu analoteua anayesalimiwa hutegemea uhusiano uliopo baina yake na anayesalimiana naye.

Pia King’ei (2010) amezungumzia rejesta ya biashara anasema kuwa madhumuni makuu ya mawasiliano katika biashara ni kuwavutia wateja na kuwafanya kuamini kuwa bidhaa ama huduma wanazouziwa ni za kiwango cha juu na za thamani bora kwa pesa zao. Hivyo lugha ya biashara (rejesta) kwa kawaida ni lugha ya kutangaza uzuri wa bidhaa au huduma huwa na sentensi fupifupi. Kwa mfano; “okoa mapesa chungu mbovu”, vilievile hutumia lugha ya kupumbaza na kuaminisha, kwa mfano: ***“kunywa XYZ kufumba na kufumbua afya yakoitakurudi****a****”***

Young, Z. (2010) alichunguza uhusiano uliopo baina ya ujumbe katika matangazo na walengwa wa ujumbe huo. Aligundua kwamba waandishi na watangazji wa matangazo ya biashara hutangaza ili waweze kujitambulisha na kutengeneza uhusiano wa karibu na watumiaji wa bidhaaa zao.

Aloo (2002) alifanya uchunguzi wa matini za matangazo ya biashara katika vituo vya televisheni na vile vya redio. Lengo lilikuwa kuchunguza mbinu za ushawishi zinazotumiwa na watangazaji katika kuendeleza biashara yao, aligundua kuwa picha, muziki na maneno yanayotumiwa na watangazaji ni vyombo muhimu vya ushawishi katika matangazo ya kibiashara.

## 2.3 Pengo la Utafiti

Utafiti huu ulipitia maaandiko kadhaa yanayohusu rejesta kama hatua ya awali ili kubaini nini kilifanyika na nini hakikufanyika. Licha ya maandiko mbalimbali kuandika na kuzungumza kuhusu rejesta ama mitindo ya lugha na lugha ya mahali fulani, kama ambavyo mapitio yalivyoonyesha, hakuna andiko lolote lililoandika kuhusu lugha inayotumika katika mazungumzo ya askari polisi. Utafiti huu ulishughulikia na kuziba pengo lililoachwa kwa kufanya utafiti katika vituo vya askari polisi kwa lengo la kuchunguza lugha inayotumika katika vituo vya askari polisi ili kubaini sifa za lugha hiyo, sababu za kutumika kwa lugha hiyo, umuhimu wa lugha hiyo katika kuitambulisha jamii ya askari polisi na mchango wa lugha ya askari polisi katika kukuza au kudumaza lugha ya Kiswahili.

## 2.4 Kiunzi cha Kinadharia

Utafiti huu ulitumia kiunzi cha Nadharia ya Rejesta cha Ghadessy na Halliday (1988). Kiunzi hiki kinafafanua uhusiano wa kimfumo ulipo kati ya muktadha na mabadiliko ya lugha yanayotokea kulingana na muktadha. Aidha, kiunzi hiki kinaitazama rejesta kama kipengele kinachofungamana na mifumo ya semantiki, sarufi na utamaduni. Vilevile rejesta inafafanuliwa na kiunzi hiki kuwa ni mtindo wa lugha unaotumika katika muktadha maalumu. Muktadha waweza kuwa ni mahali katika matini ya kimaandiko mathalani, katika kitabu, magazeti na kadhalika ambapo maudhui yatakiwayo huathiri muonekano wa matini husika.

Kwa mfano, lugha itakayotumika kuandikia kitabu cha somo la Biolojia ni tofauti na itakayotumika kuandikia somo la Historia. Hali kadhalika, muktadha mwingine, waweza kuwa mahali katika mazingira halisi ambayo si ya kimaandiko. Kwa mfano,

sokoni, mahakamani au shuleni; ambako mazungumzo kuhusu shughuli husika hufanyika. Hapa ina maana kuwa rejesta hujitokeza pia katika lugha ya maandishi mfano katika maandiko ya matini. Vilevile hujitokeza katika lugha ya mazungumzo ambayo huambatana na utamaduni wa lugha husika. Maandishi na mazungumzo ndio hutafsiriwa kuwa muktadha wa matumizi ya lugha.

Aidha, nadharia hii inafafanua kwamba lugha inayotumiwa na mwanadamu huwa imeathiriwa na muktadha unaohusika. Yaani, hakuna lugha inayotumiwa hivihivi pasipo muktadha. Muktadha huathiri matumizi ya lugha kwa kuamua namna gani lugha itumike na mahali gani au maana gani itumike na kwa nini. Pia kisemantiki maana ya vipashio vya lugha hutegemea muktadha au mahali vipashio hivyo vilimotumika, katika maandiko ya matini au mazungumzo.

Kwa mfano ili kufahamu maana ya neno (kipashio kidogo cha lugha) fulani katika andiko la matini ni sharti kuangalia mahali au sehemu neno hilo lilitumika katika sentensi iliyo ndani ya matini husika. Hali kadhalika ili kufahamu maana ya neno hilohilo katika muktadha wa mazungumzo ni sharti kuangalia mahali au sehemu neno hilo lililotumika kwa maana ya muktadha wa matumizi ya neno lenyewe.

Maelezo hayo yote yana maana kuwa neno moja laweza kuwa na maana zaidi ya moja kulingana na muktadha wa mawasiliano. Nadharia hii imetumika kutambua namna muktadha wa mazingira ya askari polisi ulivyoathiri lugha ya Kiswahili na hivyo kupata rejesta ya mazungumzo ya askari polisi jijini Mbeya.

## 2.5 Hitimisho

Sura hii iligawanyika katika sehemu tano. Sehemu ya kwanza ilihusu utangulizi.Sehemu ya pili iliangalia mapitio ya maandiko kuhusu rejesta. Sehemu ya tatu ilibainisha pengo lililoachwa na tafiti tangulizi. Aidha, kiunzi cha kinadharia kimepitiwa katika sura hii na mwisha limetolewa hitimisho la sura nzima.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaonyesha mbinu iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu. Imeeleza kwa ufasaha populesheni, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanya data, vifaa, uchambuzi wa data na mkabala uliotumika kukusanya na kuchambua data katika utafiti huu.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu kuhusu mtindo wa rejesta za askari polisi utlifanyika katika Jiji la Mbeya. Jiji la Mbeya linapatikana Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania. Kijiografia, Jiji hili lina fursa ya kupokea wageni kutoka Mal awi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Zambia. Hii ni kutokana na Mkoa wa Mbeya kupakana na baadhi ya nchi hizi na kuwa kutaniko la wafanyabiashara wanaotoka eneo la Maziwa Makuu. Wafanyabiashara hao hupitia mkoa huu wakielekea Dar es Salaam kwa shughuli za kibiashara. Eneo hili limechaguliwa kwa kuwa ni sehemu yenye mchanganyiko wa wafanyakazi kutoka katika jamii mbalimbali na mwingiliano wa Kitaifa na Kimataifa ni mkubwa kutokana na eneo lenyewe kuwa kivutio kikubwa cha biashara na upatikanaji wa vyakula vya aina mbalimbali. Mchanganyiko huo ni matokeo ya eneo hili kuwa kivutio cha uwekezaji na ajira kwa watu wengi kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania, nchi jirani na hata nje ya Bara la Afrika. Eneo hili vilevile limepitiwa na barabara kuu iendayo nchi za Rwanda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia mikoa ya Rukwa na Katavi. Kwa sababu ya mwingiliano huu kuna uwezekano wa kuwa na matumizi ya rejesta ya namna ya pekee miongoni mwa askari

polisi na ndiyo maana mtafiti amevutiwa kufanya utafiti juu ya mtindo wa rejesta za askari polisi katika eneo hili

## 3.3 Populesheni, Sampuli na Usampulishaji

Populesheni, sampuli na usampulishaji ni baaadhi ya vitu vinavyomuwezesha mtafiti kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika utafiti, vitu hivi vimefafanuliwa kama ifuatavyo:

### 3.3.1 Populesheni

Populesheni katika utafiti hurejelea idadi ya watu, makundi ya watu na vyote ambavyo mtafiti hutumia katika utafiti. Katika utafiti huu populesheni ilikuwa ni makundi ya watu wote wanaojishughulisha na kazi ya askari polisi katika jiji la Mbeya.

### 3.3.2 Sampuli

Sampuli ni sehemu ndogo ya populesheni kuu ambayo huteuliwa na mtafiti ili itumike katika utafiti wake. Aidha, Kothari (2009) anafafanua kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa kutoka katika populesheni kuu ambalo kwalo, mtafiti hupata data na kutoa hitimisho. Katika utafiti huu sampuli ni watu thelathini (30) ambao ni askari polisi (15) na askari wa usalama barabarani (15). Watafitiwa hao wamegawanyika katika makundi kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 3.1: Idadi ya Watafitiwa Katika Vituo**

| **Watafitiwa** | **Kituo cha trafiki (usalama barabarani)** | **Jumla** |
|---|---|---|
| Askari | 15 | 15 |
| Usalama barabarani | 15 | 15 |
| **Jumla** | **30** | **30** |

Chanzo: Data za Uwandani (2018)

Kama jedwali 3.1 linavyoonyesha, jumla ya watafitiwa thelathini (30), walihusishwa, yaani askari wa kituo cha polisi cha kati kumi na tano (15) askari wa usalama barabarani kumi na tano (15). Mgawanyo wa watoa habari ulikuwa kama ifuatavyo: Watoa habari kumi na tano (15) kati yao wanaume kumi (10) na wanawake watano (05) walitoka katika kituo cha polisi cha kati, watoa habari kumi na tano (15) kati yao wanaume watano (05) na wanawake kumi (10) walitoka katika kituo cha usalama barabarani (trafiki).

Kanuni;

Yamane (1967:86) alipendekeza kanuni ifuatayo iyumike kutafuta sampuli ya utafiti husika. Ambapo **n = namba ya sampuli**, **N = jumla ya watoa habari**, **e =waliokusudiwa lakini hawakutoa habari**.

Kanuni: n = N/ (1 + Ne2)

N = 44, e = 10%, n =?

n = 44 / (1+44*0.12)

n = 30

### 3.3.3 Usampulishaji

Usampulishaji ni uteuzi wa wahusika wachache kutoka katika sampuli kuu, ambao hutumika katika utafiti; na hitimisho lifikiwalo kutokana na uchache huo, huwakilisha sampuli nzima. Huu ni mchakato wa kuteua idadi fulani ya watu au vitu kutoka kwenye jamii panapofanyika utafiti kwa maana kwamba vitu au watu walioteuliwa watakuwa na sifa zitakazowakilisha jamii inayofanyiwa utafiti (Orodho na Kombo, 2002).

Utafiti huu ulitumia mbinu ya uteuzi wa sampuli kwa kigezo cha shughuli kwa sababu katika vituo vya askari polisi makundi ya watu yalikuwa mawaili ambayo ni askari polisi na jamii. Kundi la askari hujishushulisha na ulindaji wa raia na mali zao na kundi la askari wa usalama barabarani hujishughulisha na usalama wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu na abiria. Makundi ya askari polisi na askari wa barabarani ndiyo chanzo cha mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha, yaani rejesta. Usampulishaji haukuzingatia kigezo cha umri kwa sababu makundi yaliyopatikana katika vituo hivyo vya askari polisi ni ya umri unaolandana kwa vituo karibu vyote, yaani vijana kuanzia umri wa miaka 20 hadi 45. Haikuwa rahisi kwa wazee kupatikana katika vituo hivuo kwa sababu wanastaafu kwa mujibu wa sheria ya nchi.

### 3.4 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data ni jumla ya njia zote zinazotumika kukusanyia data utafiti huu ulitumia mbinu mbalimbali za kukusanyia data, tafiti, na ripoti mbalimbali zilizohusu mitindo ya lugha (rejesta).Mbinu za utafiti zinafafanuliwa na Kothari (2004) kuwa ni jumla ya mbinu zote zinazotumika katika kufanya utafiti. Mbinu za utafiti tunaweza juzigawa katika makundi mawili ambayo ni mbinu zitumikazo kukusanyia data kama vile hojaji, dodoso na ushuhudiaji na kundi la pili ni mikabala ya kuchambulia na kufafanulia data kama vile mkabala wa kiidadi na mkabala wa maelezo (usio wa kiidadi). Mbinu hizo zilitumiwa na mtafiti kupata data kwa njia ya uwandani na maktabani. Mbinu hizo zinafafanuliwa kama ifuatavyo:

#### 3.4.1 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni mchakato wa ukusanyaji wa data ambapo mtafiti hukaa na kushuhudia hali ya jambo analolitafiti na jinsi linavyotendeka kwa lengo la kukusanya taarifa.

Mbinu hii ilitumika kukusanya data katika hali ya usaili wake. Nunan (1972) anadai kuwa ili kugundua tabia fulani, mtafiti hana budi kuichunguza katika hali ya utokeaji wake. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa kwenda uwandani ambapo data zilikusanywa huku mtafitiwa akiwa na ung'amuzi bwete (yaani hakujua lolote lililokuwa likiendelea) juu ya ukusanyaji data hiyo. Hali hii ilimsaidia mtafiti kupata data asilia ambazo hazikuathiriwa kwa namna yoyote na ama mtafiti mwenyewe au mtafitiwa. Mtafiti alishuhudia mitindo ya maongezi na majibizano, yaliyokuwa baina ya askari polisi, bosi na mfanyakazi wa chini, askari polisi na watuhumiwa huku akirekodi uongeaji huo kwa kutumia kinasasauti (simu). Mbinu hii iliteuliwa kwa sababu iliweza kumpatia mtafiti taarifa kwa uasili wake, yaani data ambazo hazikuathiriwa na mtafiti au mtoa habari, vilevile mbinu hii ilichaguliwa ili kupata data zinazoaminika na kupunguza dosari zitakazo tokeza wakati wa mchakato huo.

### 3.4.2 Dodoso

Dodoso ni mbinu ya kukusanya data kwa njia ya maswali yaliyoandaliwa kabla na kujibiwa kwa maandishi. Mhojiwa hutakiwa kujibu maswali hayo kulingana na alivyoulizwa na mtafiti. Dodoso huundwa na maswali ambayo yako wazi na kuna na nafasi ya kutosha kujibia maswali (Oppenheim 2000). Dodoso zimegawanyika katika makundi mawili ambapo kuna dodoso funge na dodoso huru. Dodoso funge ni lile ambalo mtafiti hutoa orodha ya maswali yenye majibu mafupi. Kwa mfano, majibu ya NDIYO/HAPANA; wakati dodoso huru ni lile ambalo mtoa taarifa yupo huru kujibu maswali kwa maneno yake mwenyewe. Kwa mfano, Kwa nini unafikiri sheria za usalama barabarani ziendelee kutumika? Hapa mtoa taarifa yupo huru kujieleza, kwa kuwa hajawekewa mipaka kuwa aanzie wapi na aishie wapi?

Utafiti huu ulitumia aina zote mbili za maswali, yaani funge na huru. Jumla ya maswali ya dodoso yalikuwa matatu. Swalila kwanza lilimtaka kila mtoa habari kutaja msamiati/maneno matano (05) yaliyokuwa yakitumika katika vituo vya kazi vya askari polisina aeleze maana kwa kila msamiati alioutaja. Swali la pili lilimtaka mtoa habari kueleza kazi za rejesta katika.mawasiliano ya askari polisi na swali la tatu lilimtaka mtoa habari kutaja sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta katika mawasiliano ya askari polisi. Dodoso hilo lilimsaidia mtafiti kujibu maswali yote yaliyohusu utafiti huu. Sababu ya kuchagua mbinu hii ya dodoso ni kwamba inaweza kumsaidia mtafiti kupata taarifa za utafiti kutoka kwa baadhi ya watoa habari ambao hawako tayari kujulikana kuwa wamechangia taarifa katika utafiti husika.

### 3.4.3 Mahojiano/Usaili

Mbinu ya mahojiano inahusisha maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa lengo la kupata taarifa ya jambo fulani. Maswali haya huulizwa kwa mdomo na majibu yake yaweza kurekodiwa katika daftari au tepurekoda.

Kwa mujibu wa Kombo na Trompo (2006) mahojiano ni mbinu ya majibizano ya ana kwa ana (au ya simu, barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Kuna aina mbili za usaili, yaani funge na huru. Katika usaili funge mtafiti huuliza maswali kama yalivyoandikwa katika karatasi na si nje ya hayo. Katika usaili huru mtafiti yuko huru kuuliza maswali ya ziada na wakati mwingine kutokuuliza baaadhi ya maswali aliyoyaandaa pale anapoona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo. Mtafiti aliweza kukutana na watafitiwa thelathini (30).

Utafiti huu ulitumia usaili wa aina zote mbili yaani funge na huru. Jumla ya masali yaliyokuwepo kwenye hojaji yalikuwa matatu. Kwa kutumia usaili funge mtafiti aliwauliza watafitiwa maswali yote kama yalivyoandikwa katika karatasi. Kwa usaili huru mtafiti alimuuliza mtafitiwa mmoja swali ambalo halikuwepo kwenye hojaji ambalo liliuliza "je, matumizi ya rejesta hii yanasaidia kuleta ufanisi katika kazi yenu" Vilevile mwanya wa maswali tokezi au ibukizi (yaani maswali yanayotokea katikati ya majadiliano) uliachwa wazi ili kuwaruhusu wahojiwa kujieleza zaidi. Mbinu hii iliteuliwa kutumika kwa sababu zifuatazo:

Kwanza ilikuwa rahisi kwa mtafiti kudhibiti sampuli kwa usahihi zaidi. Hii iliwezekana kwa sababu mtafiti alikutana na wahojiwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kuyarekodi majibu yao. Hivyo maswali yaliyokosa majibu yalitafutiwa ufumbuzi papo kwa papo.

Pili ilikuwa ni rahisi kwa mtafiti kukusanya taarifa nyingi na kwa kina zaidi, kwa sababu alikuwa na uhuru wa kuuliza maswali ya ziada(maswali tokezi) ambayo ni vigumu kufanyika kwa kutumia njia nyingine na sababu ya tatu ni kwamba, ilikuwa rahisi kwa watafitiwa kumuuliza mtafiti maswali ambayo hawakuyaelewa na mtafiti aliwaelewesha. Hali hii ilimsaidia mtafiti kupata data stahiki kutoka kwa watafitiwa.

## 3.5 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wa data (Kothari, 2004). Utafiti huu ulitumia **vifaa**kama vile, kompyuta, simu ya mkononi, shajara na kalamu. Vifaa hivi na jinsi vilivyotumika vinajadiliwa kama ifuatavyo:

### 3.5.1 Simu ya Mkononi

Simu ya mkononi nikifaa ambacho hutumika katika mawasiliano, lakini mbali na kutumika kama chombo cha mawasiliano simu ina kazi mbalimbali ikiwemo ya kuandika na kutunza kumbukumbu. Taarifa zilikusanywa kwa njia ya kunasa sauti, mitindo ya lugha iliyokuwa ikitumiwa na askari polisi na baadaye kuitolea maelezo katika kipengele cha uchanganuzi. Vilevile maelezo, majibizano na mahojiano mbalimbali kati ya mtafiti na watafitiwa yalirekodiwa kwa njia ya simu.

### 3.5.2 Shajara na Kalamu

Shajara ni kitabu kinachotumika kuandikia kumbukumbu za matukio ya kila siku (TUKI 2004:356). Hapa mtafiti alilazimika kutumia kalamu na shajara ili kurekodi majina ya maeneo yaliyohisika katika utafiti wake, taarifa za watu mbalimbali waliohusika katika utafiti pamoja na kuandikia na kutunzia mitindo mbalimbali ya usemaji iliyokusanywa katika vituo vya kazi vya askrari polisi.

Mtafiti alivitumia vifaa hivi pale alipokuwa katika vituo vya askari polisi akikusanya data na hasa kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji. Vilevile alivitumia kuandikia taarifa nyingine ambazo aliona kuwa zinaweza kumsaidia kupata data alizozihitaji.

### 3.5.3 Kompyuta

Kompyuta pia ilitumika pia katika mambo mengi ili kufanikisha utafiti huu. Ilitumika katika kuandika, kuchanganya maandishi na picha, maandishi na vielelezo mbalimbali, kuhifadhi kumbukumbu zilizorekodiwa uwandani na kadhalika. Yote haya yamewezekana kwa kutumia kompyuta.

### 3.6 Uchambuzi wa Data

Katika zoezi la kuchambua data mikabala mbalimbali hutumika kama vile mkabala wa kiidadi na mkabala wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Williman (keshatajwa) mkabala wa kiidadi ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data kwa kutumia namba ili kurekodi taarifa na kuwasilisha kwa njia ya takwimu. Naye, Enon (1998) anaeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchambua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo. Kutokana na aina ya kazi yake, mtafiti alikusudia kutumia mikabla yote miwili.

### 3.7 Changamoto za Ukusanyaji wa Data

Zipo changamoto kadhaa ambazo mtafiti alikabiliana nazo katika ukusanyaji wa data, changamoto hizo ni kama vile, baadhi ya watafitiwa hawakurudisha hojaji na dodoso kwa wakati alioupanga mtafiti. Pia watafitiwa wengine waliiona kazi hii ya utafiti kama ni kuchunguza kazi za askari polisi.

### 3.8 **Hitimisho**

Sura hii kwa ujumla imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika kupata data, eneo la utafiti, sampuli lengwa na mbinu iliyotumika kuwasilisha data zilizokusanywa toka uwandani. Ingawa kuna changamoto zilizojitokeza katika ukusanyaji data, changamoto hizo hazikuathiri upatikanaji wa data za kutosha na kuaminika kutoka kwa watafitiwa. Mtafiti aliridhika na data zilizokusanywa uwandani kwa sababu ilikidhi malengo ya utafiti. Kwa hiyo data zote zilizokusanywa zimewasilishwa kwa upana katika Sura ya Nne, inafuata baada ya sura hii ya Tatu.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imewasilisha matokeo ya data zilizokusanywa kutoka uwandani zinazohusu mtindo wa lugha unaojulikana kama rejesta ambao unatumika katika vituo vya kazi vya askari polisi katika jiji la Mbeya. Data zote zimewasilishwa kulingana na malengo ya utafiti na maswali yake. Uwasilishaji wa data kwa ujumla uliongozwa na kiunzi cha Ghadessy na Halliday (1988) kinachohusu rejesta. Kiunzi hiki kinafafanua uhusiano wa kimfumo uliopo kati ya muktadha na lugha inayotumika katika muktadha huo.

**Jedwali 4.1: Msamiati Uliopatikana Toka Kwa Askari Polisi na Askari wa Usalama Barabarani**

| Na | Msamiati | Maana yake katika rejesta ya askari Polisi |
|---|---|---|
| 1 | Afande | Alfa Fox Alfa November Delta Echo |
| 2 | Lindo | Lima India November Delta Osca |
| 3 | Mlalamikaji | Mike Lima Alfa Lima Alfa Mike India Kilo Alfa Juliety India |
| 4 | Mshitakiwa | Mike Siela Hotel India Tango Alfa Kilo India Wisky Alfa |
| 5 | Shahidi | Siela Hotel Alfa Hotel India Delta India |
| 6 | Kituoni | Kilo India Tango Uniform Osca November India |
| 7 | Haraka | Hotel Alfa Romeo Alfa Kilo Alfa |
| 8 | Nimekusoma | November India Mike Kilo Echo Kilo Uniform Siela Osca Mike Alfa |
| 9 | Nitatekeleza | November India Tango Alfa Tango Echo Kilo Echo Lima Echo Zulu Alfa |
| 10 | Sheria | Siela Hotel Echo Romeo India Alfa |
| 11 | Barabara | Bravo Alfa Romeo Alfa Bravo Alfa Romeo Alfa |
| 12 | Ndiyo | November Delta India Yankee Osca |
| 13 | Polisi | Papa Osca Lima India Siela India |
| 14 | Mkamateni | Mike Kilo Alfa Mike Alfa Tango Echo November India |
| 15 | Kesi | Kilo Echo Siela India |
| 16 | Vunja | Victa Uniform November Juliety Alfa |
| 17 | Unyanyasaji | Uniform November Yankee Alfa November Yankeee Alfa Siela Alfa Juliety India |
| 18 | Leseni | Lima Echo Siera |
| 19 | Jinai | Juliety India November Alfa India |
| 20 | Dereva | Delta Echo Romeo Echo Victa Alfa |

Chanzo: Data za Utafiti 2017

## 4.2 Watoa Habari

Jumla ya watafitiwa 30 kutoka vituo vya kazi vya askari polisi 2 katika jiji la Mbeya walifanyiwa utafiti ambapo 15 walitoka katika kituo cha polisi cha kati na 15 walitoka katika kitu cha polisi wa usalama barabarani.

## 4.3 Kiwango cha Rejesta Matumizi ya Rejesta Askari Polisi

Katika jeshi la polisi, rejesta zinafanana lakini kuna utofauti ndogo kutokana na kazi ambazo hufanywa na haya majeshi. Kwa mantiki hiyo, ufuatao ni uchambuzi wa rejesta unaotumika katika vituo vya kazi vya askari polisi:

### 4.3.1 Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi

Katika swali hili, dodoso liligawiwa kwa askari polisi 15. Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubaini namna rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa katika vituo vya kazi vya askari polisi. Kutokana na swali la kwanza lililouliza je ni kwanamna gani rejesta ya askari polisi huzungumzwa*?* Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia njia ya dodoso na mahojiano kwa kutumia usampulishaji tegemea fursa ambapo wahojiwa hao walikuwa na majibu yaliyobainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.2: Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta za Askari Polisi**

| Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya rejesta za askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Afande | 5 | 33 |
| Lindo | 3 | 20 |
| Mlalamikaji | 2 | 13 |
| Mshitakiwa | 4 | 27 |
| Shahidi | 1 | 07 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti 2017

Kutokana na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa katika watoa habari (askari polisi) 15, watoa habari 5 (33%) walisema kuwa neno Lindo ni miongoni mwa maneno rejesta yanayotumika mara nyingi zaidi katika jeshi la polisi, watoa habari 3 (20%) walisema kuwa neno afande hutumika mara nyingi zaidi katika mazungumzo ya askari polisi, pia watoa habari 2 (13%) walisema kuwa neno mlalamikaji hutumiwa katika rekodi za askari, vilevile watoa habari 4 (27%) walisema kuwa neno mshitakiwa hutumika katika kazi ya askari polisi . Pamoja na data hizo mtoa habari mmoja (07%) alithibitisha kuwa neno mtuhumiwa linatumika katika kazi ya askari polisi.

Mtafiti alifanya mahojiano Na askari polisi kutoka kitengo cha mawasiliano kuhusuneno Lindo, askari huyo alieleza kuwa neno **lindo** katika rejesta ya askari polisi linatamkwa*"**Lima India November Delta Oska"***, rejesta hii inamaanisha kwamba sehemu ambayo askari polisi wanalinda raia na mali zao (chanzo, data za utafiti, 2017)

**Jedwali 4.3: Kubainisha Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi**

| Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Kituoni | 4 | 27 |
| Haraka | 1 | 07 |
| Nimekusoma | 3 | 20 |
| Nitatekeleza | 5 | 33 |
| Sheria | 2 | 13 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na data zilizopo katika Jedwali 4.3, data zilizopatikana uwandani zinaonyesha kuwa, matokeo ya watoa habari 4 (27%) walidhihirisha matumizi ya neno kituoni katika lugha ya askari polisi pale ambapo mmoja wao anapomuagiza mwingine ampeleke mtuhumiwa kituoni, mtoa habari 1 (07%) alisema kuwa neno haraka hutumika pale askari polisi wa ngazi ya juu anapomwita askari wa ngazi ya chini, watoa habari 3 (20%) walisema neno nimekusoma linatumika wakati wa mawasiliano ya rediocall likimaanisha taarifa au agizo lililotolewa limeeleweka, pia watoa habari 5 (33%) walidhihirisha neno nitatekeleza hutumika wakati askari wa ngazi ya juu anapoagiza kazi kwa askari wa ngazi ya chini, watoa habari2 (13%) walisema kuwa neno njoo hutumika katika mazungumzo ya askari polisi wawapo kazini.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kutoka kitengo cha mapokezi kuhusu neno kituoni hutumika mara nyingi zaidi na askari polisi kwa sababu ndio mahali ambapokazi nyingi hufanyika hapo, askari huyo alieleza kuwaneno***kituoni***katika rejesta yaaskari polisi linatamkwa*“**Kilo India Tango Uniform Osca November”*** rejesta hiiinamaanisha sehemu ambayo askari polisi wanapokea taarifa ambalimbali za kihalifupamoja na wahalifu. (Chanzo, data za utafiti, 2017).

**Jedwali 4.4: Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi**

| Kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Barabara | 2 | 13 |
| Ndiyo | 1 | 07 |
| Polisi | 2 | 13 |
| Mkamateni | 4 | 27 |
| Kesi | 6 | 40 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutoka na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa watoa habari 2 (13%) walidhihirisha uwepo wa neno barabara katika mazungumzo ya askari polisi, pia mtoa habari 1 (07%) alisema neno ndiyo ni miongoni mwa maneno yanayotumika katika jeshi la askari polisi, Vilevile neno watoa habari 4 (27%) walibainisha namna neno mkamateni linavyotumika katika lugha yao. Aidha watoa habari 6 (40%) Walidhihirisha namna neno kesi linavyotumika katika lugha hiyo.

Mtafiti alifanya mahojiano Na askari polisikutoka kitengo cha mawasiliano kuhusuneno kesi, askari huyo alieleza kuwa neno***kesi***katika rejesta ya askari polisilinatamkwa*"**kilo EchoSiera India"***, rejesta hii inamaanisha kwambatuhuma zinazomkabili mtu *(*chanzo, data za utafiti, *2018).*

**Jedwali 4.5: Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi**

| Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Vunja | 5 | 33 |
| Unyanyasaji | 4 | 27 |
| Leseni | 2 | 13 |
| Jinai | 3 | 20 |
| Dereva | 1 | 07 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na data zilizoonyeshwa katika Jedwali 4.5, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa watoa habari 5 (33%) walibainisha kuwa neno vunja linatumika wakati raia wanapofika kutoa taarifa juu ya tukio la kihalifu lililotokea, pia watoa habari 4 (27%)

walisema kuwa neno unyanyasaji linatumika mara kwa mara pale ambapo askari polisi wanapopewa taarifa za unyanyasaji wa matukio mbalimbali, watoa habari 2 (13%) walidhihirisha kuwa neno Leseni linatumika katika lugha hiyo wakati madereva wanapofika kushughulikia leseni zao zinazowatambulisha kuwa wamepitia mafunzo ya kuendesha vyombo vya moto,  mtoa habari 1 (07%) alithibisha kuwa neno dereva pia ni miongoni mwa maneno yanayotumika katika lugha hiyo ya askari polisi.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kutoka kitengo cha mawasiliano kuhusu neno Lindo, askari huyo alieleza kuwa neno***vunja***katika rejesta ya askari polisilinatamkwa*“**Victa Uniform November Juliety Alfa”***, rejesta hii inamaanisha kwamba sehemu wahalifu walienda kuvamia kinyume nasheria (chanzo, data za utafiti, 2017).

Hitimisho

### 4.3.2 Kiwango na Matumiziya Rejesta ya Askari Polisi Wa Usalama Barabarani Zinavyozungumzwa

Katika swali hili, askari polisi wa usalama barabarani walikuwa na maoni tofauti na askari polisi. Lengo la uwasilishaji huu ni kutaka kubainisha namna rejesta ya askari polisi wa usalama barabarani zinavyozungumzwa lengo hili linaenda sambamba na swali la kwanza la utafiti lililouliza, je ni kwa namna gani rejesta ya askari polisi huzungumzwa? Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia njia ya dodoso na mahojiano kwa kutumia usampulishaji tegemea fursa ambapo watoa habari 15 walipatikana na kutoa majibu katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.6: Data zaidi Zionyeshazo Kiwango cha Matumizi ya Rejesta za Askari Polisi wa Usalama Barabarani**

| Kiwango cha matumizi ya rejesta za askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Dereva | 6 | 40 |
| Lindo | 4 | 27 |
| Mlalamikaji | 2 | 13 |
| Mshitakiwa | 2 | 13 |
| Shahidi | 1 | 07 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2018)

Kutokana na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa watoa habari 6 (40%) walidhihirisha uwepo wa neno dereva katika mazungumzo ya askari wa usalama barabarani, pia watoa habari 4 (27%) walisema neno lindo ni miongoni mwa maneno yayotumika katika jeshi la askari wa uasalama barabarani, watoa habari 2 (13%) nao walisema kuwa neno mlalamikaji hutumika katika kazi ya askari polisi, Vilevile watoa habari 2(13%) walibainisha namna neno mshitakiwa linavyotumika katika lugha yao. Aidha watoa habari 1(07%) walidhihirisha namna neno shahidi linavyotumika katika lugha hiyo.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari wa usalama barabarani polisi kutoka point A kuhusu neno dereva, askari huyo alieleza kuwa neno***dereva***linatumika mara nyingizaidi katika kutekeleza majukumu yao kwa rejesta ya askari polisi linatamkwa *"**Delta Echo Romeo Echo Victa Alfa**"*, rejesta hii inamaanisha mtu anayeendesha vyombovya usafiri (chanzo, data za utafiti, 2017).

Hitimisho

**Jedwali 4.7: Data zaidi za Kiwango cha Matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani**

| **Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa** | **Idadi** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Kituoni | 5 | 33 |
| Haraka | 1 | 07 |
| Nimekusoma | 1 | 07 |
| Nitatekeleza | 2 | 13 |
| Sheria | 6 | 40 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na data zilizopo katika Jedwali 4.3, data zilizopatikana uwandani zinaonyesha kuwa, matokeo ya watoa habari 5 (33%) walidhihirisha matumizi ya neno kituoni katika lugha ya askari polisi pale ambapo mmoja dereva anaposababisha ajali hupelekwa kituoni, mtoa habari 1 (07%) alisema kuwa neno haraka hutumika pale askari polisi wa napohitajika kuwahi katika eneo la tukio, mtoa habari 1 (07%) alisema neno nimekusoma linatumika wakati wa mawasiliano ya rediocall likimaanisha taarifa au agizo lililotolewa limeeleweka, pia watoa habari 2(13%) walidhihirisha neno nitatekeleza hutumika wakati askari wa ngazi ya juu anapoagiza kazi kwa askari wa ngazi ya chini, watoa habari6 (40%) walisema kuwa neno sheria hutumika wakati wa kutoa taarifa za uvunjaji wa sheria za barabarani.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kutoka kitengo cha mawasiliano kuhusu neno kituoni, askari huyo alieleza kuwa neno ***kituoni***linatumika marakwa mara pale ambapo dereva anaposhindwa kutimiza yale aliyoambiwa na askari, katika rejesta ya askari polisi linatamkwa*"**Kilo Tango Uniform Osca November India**, rejesta hii* inamaanisha kwamba sehemu ambayo askari polisi wanapokea wanafanya shughuli za

ulinzi wahalifu taarifa zinazohusu wahalifu haotaarifa zinazohusu wahalifu hao(chanzo, data za utafiti, 2017).

**Jedwali 4.8: Kiwango na matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani**

| Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Barabara | 6 | 40 |
| Ndiyo | 1 | 07 |
| Polisi | 2 | 13 |
| Mkamateni | 3 | 20 |
| Kesi | 3 | 20 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutoka na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa watoa habari 6 (40%) walidhihirisha uwepo wa neno barabara katika mazungumzo ya askari polisi, pia mto habari 1 (07%) alisema neno ndiyo ni miongoni mwa maneno yayotumika katika jeshi la askari polisi, watoa habari 2 (13%) nao walisema kuwa neno polisi hutumika katika kazi ya askari polisi, Vilevile watoa habari 3 (20%) walibainisha namna neno mkamateni linavyotumika katika lugha yao. Aidha watoa habari 3(20%) Walidhihirisha namna neno kesi linavyotumika katika lugha hiyo.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kutoka pointi B kuhusu neno barabarani, askari huyo alieleza kuwa neno ***barabarani*** linatumika mara kwa mara kwa sababundio moja ya sehemu ambazo hutimizia utekelezaji wa kazi zao, katika rejesta *ya* askari polisi linatamkwa ***"Bravo Alfa Romeo Alfa Bravo Alfa Romeo Alfa November India****",* rejesta hii inamaanisha mahali ambapo watu na vyombo vya moto hupita. (Chanzo, data za utafiti, 2017).

**Jedwali 4.9: Data zaidi za Kiwango na matumizi ya Rejesta ya Askari Polisi wa Usalama Barabarani**

| Kubainisha kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi zinavyozungumzwa | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Vunja | 4 | 27 |
| Unyanyasaji | 2 | 13 |
| Leseni | 5 | 33 |
| Jinai | 1 | 07 |
| Kupima | 3 | 20 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na data zilizoonyeshwa katika Jedwali 4.5, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa watoa habari 4 (27%) walibainisha kuwa neno vunja linatumika wakati raia wanapofika kutoa taarifa juu ya tukio la kihalifu lililotokea, pia watoa habari 2 (07%) walisema kuwa neno unyanyasaji linatumika mara kwa mara pale ambapo askari polisi wanapopewa taarifa za unyanyasaji wa matukio mbalimbali, watoa habari 5 (33%) walidhihirisha kuwa neno Leseni linatumika mara nyingi wakati askari wanapofanya ukaguzi leseni zao zinazowatambulisha kuwa wamepitia mafunzo ya kuendesha vyombo vya moto, mtoa habari 1 (07%) alithibisha kuwa neno jinai pia ni miongoni mwa maneno yanayotumika katika lugha hiyo ya askari polisi, vilevile 3 (20%) walithibitisha kuwa neno dereva halikwepeki katika mazungumzo yao wawapo kazini.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kutoka pointi D alieleza kuwa neno***leseni***linatumika mara nyingi zaidi katika kazi yao sababu ndio moja ya kazi zao ni ukaguzi wa leseni, katika rejesta ya askari polisi linatamkwa ***"Lima Echo Siela***

***Echo NovemberIndia",*** rejesta hii inamaanisha hati ya kitambulisho inayoonesha muhusikaamepata mafunzo ya udereva.(Chanzo, data za utafiti, 2017).

Hivyo, kutokana na data zilizopatikana imeonekena kuwa kiwango cha matumizi ya rejesta ya askari polisi katika mazungumzo yao ni kikubwa kwa lengo la kuwatambulisha wao wenyewe. Matokeo hayo yameonyesha kufanana na utafiti wa Young (keshatajwa) ambaye katika utafiti wake aligundua kuwa watangazaji wa biashara hutangaza ili waweze kujitambulisha na kutengeneza uhusiano wao wa karibu.

## 4.4 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi

Katika lengo la pili la utafiti huu, wahojiwa (askari polisi na askari usalama barabarani) walikuwa na maoni tofauti katika kuelezea kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi. Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi kuhusu kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi.

### 4.4.1 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi

Katika lengo hili, dodoso liligawiwa kwa askari polisi 15. Lengo la uwasilishaji huu ni kutaka kufahamu kazi za rejesta katika mawasiliano ya askari polisi, lengo hili linaenda sambamba na swali la pili la utafiti huu lililouliza, je nini kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi wa jiji la Mbeya? Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia njia ya dodoso na mahojiano kwa kutumia usampulishaji tegemea fursaambapo watoa habari waliopatikana walikuwa na majibu yaliyobainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.10: Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari Polisi**

| **Kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari Polisi** | **Idadi** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|
| Je, rejesta hutumika kufisha siri | 6 | 40 |
| Je, rejesta hutumika katika kupunguza Idadi ya maneno | 1 | 07 |
| Rejesta hutumika kurahisisha mazungumzo | 4 | 27 |
| Je, rejesta ni kitambulisho cha mzungumzaji | 2 | 13 |
| Je, rejesta hutumika kupamba lugha | 2 | 13 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na takwimu ilizopo katika Jedwali 4.10 zilizopatikana uwandani, motokeo ya utafiti yalionyesha kuwa watoa habari 6 (40%) walithibitisha kuwa rejesta hutumika kuficha usiri, mtoa habari 1 (7%) alibainisha kuwa rejesta humika katika kupunguza idadi ya maneno, watoa habari 4 (27%) walisema kuwa rejesta hutumika kurahisisha mazungumzo wawapo kazini, watoa habari 2 (13%) walibainisha kuwa rejesta ni kitambulisho cha mzungumzaji katika kutofautisha ngazi ya kazi, watoa habari 2 (13%) walisema pia rejesta hutumika kupamba lugha.

Mtafiti alifanya mahojiano na watoa taarifa kutoka kitengo cha mawasiliano kuhusukazi ya rejesta ya askari, askari hao walieleza kuwa moja ya kazi za rejesta ya askari polisi ni ***"kuficha usiri"***pale ambapo askari polisi wanapowasiliana bila mtu aliye pembeni yao kuelewa maana ya mtindo wa lugha wanaotumia. *"Victa* ***India Papa India, IndiaLima Echo Kilo Echo Siela India***" rejesta hiyo ina maana "Vipi ile kesi" mfano huo unaonyesha jinsi polisi wanavyoweza kuwasiliana bila mtu mwingine asiye askari kufahamuwanachoongea, (Chanzo, data za utafiti, 2018).

Pia mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi 1 (07%) wa kitengo cha upepelezi alisema kuwa kazi ya rejesta ya askari polisi ni pamoja na **kupunguza idadi ya**

**maneno** ambapo hutokea tu wakati wakiendelea na shughuli zao hutumia mtindo huo wa lugha yao kwa kuifupisha. Kama vile wanapokuwa wameenda nyumbani kwa mtu kufanya upekuzi kwa ajili ya uchunguzi juu ya tukio fulani, baada ya uchunguzi huo hukuta hamna kitu cha kusaidia upelelezi wao. Kwa mfano,"askari mwenye cheo anawauliza walio wadogo kuhusu taarifa za pekuzi wale askri hujibu ***"NIL"*** maana yake hawakufanikiwa kupata kielelezo chochote.

Katika utafiti huu, Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi 4 (27%) kutoka kitengo cha mapokezi walieleza kuwa kazi nyingine ya rejesta ya askari polisi ni **kurahisisha mawasiliano wawapokazini,** walisema kuwa kutokana na umuhimu wa kazi yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao huona ni vizuri zaidi wakitumia mtindo wa lugha ambayo itawajumuisha wao tu na hivyo hata kazi yao kuwa salama zaidi. Kwa mfano: "***Afande November Juliety Osca Osca Chalii"***Ina maana kuwa afande husika anatakiwa aende kituo cha polisi cha kati (central).

Vilevile mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi 2 (13%) walieleza kuwa rejesta ya askari polisi hutumika kama **utambulisho wa wafanyakazi wa jeshi la polisi** kwa kuwatofautisha na kundi jamii lingine kwa kuwa ni vigumu kwa mtu aliye nje ya jeshi la polisi kutumia mtindo huo wa lugha, walisema kuwa kwa sababu kundi hili ni muhimu sana kwa jamii kwa ajili ya kulinda usalama wa raia na mali zao hutumika pia kutambuana wanapokuwa katika harakati za kupambana na wahalifu.

Aidha mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi 2 (13%) walisema kuwa rejesta ya askari polisi hutumika **kupamba lugha** pale wanapoitumia mtu asiye askari polisi anapoisikiliza majibizano yanayoendelea huonekana kama mchezo fulani wa

kufurahisha, hivyo hupelekea kuvutiwa kusikiliza namna wanavyozungumza ingawa hawezi kuelewa kinachozungumzwa. Kwa mfano ***"Njoo chalii IM"***ina maana njoo kituo cha polisi haraka sana, ***"Nimekusoma 5/5"***ina maana nimekuelewa kwa utekelezaji. Mifano hiyo inaonyesha mawasiliano kati ya askari polisi, lakini masikioni mwa mtu mwingine asiye katika sekta ya jeshi la polisi ataona kama ni mchezo fulani unaovutia kusiliza.

### 4.4.2 Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari wa Usalama Barabarani

Askari wa usalama barabarani wao walikuwa na maoni tofauti walipoulizwa swali hilohilo kuhusu kuelezea kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari wa usalama barabarani. Katika swali hili, dodoso liligawiwa kwa askari wa usalama barabarani 15. Lengo la uwasilishaji huu ni kutaka kufahamu kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari wa usalama barabarani, lengo hili linaenda sambamba na swali la pili lililouilza, je nini kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi wa jiji la Mbeya? Data zilikusanywa kupitia njia ya dodoso na mahojiano kwa kutumia usampulishaji tegemea fursa, majibu yao yamebainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.11: Data zaidi Kuhusu Kazi ya Rejesta Katika Mawasiliano ya Askari wa Usalama Barabarani**

| Kueleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari Polisi | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Je, rejesta hutumika kufisha siri? | 5 | 33 |
| Je, r ejesta hutumika katika kupunguza Idadi ya maneno | 2 | 13 |
| Rejesta hutumika kurahisisha mazungumzo | 3 | 20 |
| Je, rejesta ni kitambulisho cha mzungumzaji | 4 | 27 |
| Je, rejesta hutumika kupamba lugha | 1 | 07 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na takwimu zilizopo katika Jedwali 4.11 zilizopatikana uwandani, motokeo ya utafiti yalionyesha kuwa watoa habari 5 (33%) walithibitisha kuwa rejesta hutumika kuficha usiri, watoa habari 2 (13%) walibainisha kuwa rejesta humika katika kupunguza idadi ya maneno, watoa habari 3 (30 %) walisema kuwa rejesta hutumika kurahisisha mazungumzo wawapo kazini, watoa habari 4 (27%) walibainisha kuwa rejesta ni kitambulisho cha mzungumzaji katika kutofautika ngazi ya kazi, mtoa habari 1 (07%) walisema pia rejesta hutumika kupamba lugha.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari wa usalama barabarani 5 (33%) walieleza kuwa kazi ya rejesta ya askari polisi ni***kuficha usiri***ili kuwatenga watu wengine wasiokatika kitengo cha usalama barabarani, walisema kuwa wakati mwingine wanapokuwa katika mazingira ya kazi huona ni vema kutumia mtindo wa lugha yao(rejesta) ili kazi yao iende vizuri, kwa mfano neno*"**Juliety Alfa Mike Bravo Osca**"* afandemaana yake Jambo Afande, "kuna mtu nimempa ***kihusuka chako***", ina maanakuna mtu nimempa namba yakoya simu, (Chanzo, data za utafiti, 2017).

Pia mtafiti alifanya mahojiano na askari wengine wa uaslama barabarani 2(13%) walisema kuwa kazi nyingine ya rejesta yaaskari polisi ni **kupunguza idadi ya maneno** ambapo walieleza kuwa katika harakati za utekelezaji wa majukumu yao wawapo katika vituo vya kazi ambavyo hupangiwa kila baada ya wiki moja hubadilishwa kwenda kituo kingine huhitaji mawasiliano ya haraka kutoka kituo kimoja hadi kituo kingine A kwenda pointi B. Kwa mfano Afande mmoja anapompigia simu mwenzake kumweleza kuwa zamu yake kwa siku husika imekwisha hivyo anaenda nyumbani.Anampigia akisema afande naelekea "***Hotel Mike (H & M)"*** hii iana maaana anaelekea nyumbani.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari wa usalama barabarani 3 (20%) walisema kuwa rejasta ya askari polisi pia hutumika **kurahisisha mawasiliano** katika utendaji wao wa kazi hasa pale dereva aliyesimamishwa point A anapogoma kusimama, hivyo askari walio pointi A wanawasiliana kwa haraka na wale walio katika poiniti B Ili wamsimamishe dereva husika. Kwa mfano "simamisha "***Gofu Alfa Romeo India, November Alfa T 317 BNW***" ina maana simamisha gari namba T317 BNW.

Vilevile mtafiti alifanya mahojiano na askari wa usalama barabarani 4 (27%) walieleza kuwa kazi mojawapo yarejesta ya askari polisi ni **kumtambulisha mzungumzaji kwa ngazikutokangazi ya juu hadi kazi ya chini**. Walisema kuwa kwa kawaida jeshi la polisi hutoa utambulisho ambao humtambulisha kiongozi husika wa himaya hiyo.

Kwa mfano, "Kanga 1: ***Control kwa kanga 1***

Control: Nakupata ***Kanga 1***

Kanga 1: ***Niitie kanga 3***

Walisema kuwa kanga 1 ni mkuu wa polisi wa wilaya, Kanga 3 ni mkuu wa usalama barabarani hivyo basi rejesta yao imetumuika kuwatofautisha. Aidha mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa usalama barabarani 1 (07%) alieleze kuwa rejesta ya askari polisi huweza kutumika **kupamba lugha** na kuonekana inavutia wakati askari hao wanapowasiliana wakiwa katika vituo vyao vya kulinda usalama wa barabarani na watu wasio jamii lugha hiyo wakisikia hutamani kusikia zaidi.

Kwa mfano:***"point A mlete huyoDeltaEcho Romeo Echo Victa Alfa hapa point B"*** ina maana askari aliye point A anaitwa ampeleke dereva husika Pointi B***,"Rojaafande"*** ina maana sawa afande natekeleza.

Hivyo, kutokana na data hizo imeonekana kuwa matokeo ya utafiti huu yanafanana na utafiti wa Mbunda (keshatajwa) alichunguza rejesta ya hotelini ambapo utafiti wake ulionesha kuwa kuna mfanano wa kazi za rejesta zao kama vile kurahisisha mawasiliano miongoni mwao na kupamba lugha.

## 4.5 Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi

Katika lengo la tatu la utafiti huu, wahojiwa (askari polisi na askari usalama barabarani) walikuwa na maoni tofauti katika kuelezea sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi.

### 4.5.1 Maelezo kuhusu Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi

Katika swali hili, dodoso liligawiwa kwa askari polisi 15. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kutaka kufahamu sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi, lengo hili linaenda sambamba na swali la tatu la utafiti lililouliza,je ni sababu zipi zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi? Data za utafiti huu zilikusanywa kupitia njia ya mahojiano kwa kutumia usampulishaji tegemea fursa ambapowahojiwa hao walikuwa na majibu ambayo yamebainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.12: Data zaidi za Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari Polisi**

| Maelezo kuhusu sababu za ukuaji wa rejesta ya askari polisi | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Kutunza taarifa ili zisivuje kwa mtu mwingine kabda upelelezi haujakamilika | 6 | 40 |
| Kumficha adui | 4 | 26 |
| Matumizi ya kila siku | 1 | 7 |
| Uwepo wa matukio ya uvunjanji wa sheria za usalama barabarani | 1 | 7 |
| Uwepo wa shughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani kama vile ajali inayohusisha magari | 3 | 20 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa kitengo cha upelelezi 6 (40%), askari hao walisema moja ya sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ni **kutunza taarifa ili zisivuje kwa mtumwingine kabda upelelezi haujakamilika**. Hivyo alieleza kwamba askari wa upelelezi anapokuwa katika shughuli hiyo kuna wakati hulazimika kutumia rejesta yao mara anapowasiliana na mkuu wake wa kazi ambaye alimwagiza kufanya kazi husika.

Vilevile mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa kitengo cha mawasilino askari huyo alieleza kuwa sababu inayopelekea ukuaji ya rejesta hii ni **kumficha adui** 4 (26%), alifafanua kuwa askari polisi wanapokuwa mitaani kushughulikia tukio la uvamizi fulani unaohusisha matumizi ya silaha kati yao na wahalifu, askari huwasiliana kwa rejesta ili adui asitambue maelekezo waliyopewa.

Mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa kitengo cha mapokezi, yeye alisema kuwa sababu zinazopelekea **ukuaji wa rejesta yao ni matumizi ya kila** siku 1 (7%), alieleza kuwa katika kitengo chao cha mapokezi kila siku wanapokea taarifa zinazohusu mashitaka mbalimbali pamoja na watuhumiwa wa kesi mbalimbali. Hivyo katika kutekeleza majukumu hayo wao hulazimika kutumia rejesta hii ili kazi yao iwe salama zaidi.

Pia mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa usalama barabarani, askari huyo alisema kuwa sababu zinapelekea ukuaji wa rejesta ya askari polisi ni **uwepo wa matukio ya uvunjanji washeria za usalama barabarani** 1 (7%), alifafanua kuwa pale inapotokea dereva amevunja sheria labda amesababisha ajali, askari husika anapotoa taarifa kwa mkuu wake wa kazi kwa kutumia redio call hutumia rejesta yao.

Aidha mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa usalama barabarani katika pointi nyingine ya ulinzi, yeye alieza kuwa sababu inayopelekea ukuaji wa rejesta ya askari poilisi ni **uwepo washughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani** kama vile ajali inayohusisha magari tu inapotokea askari huitwa na wanapima ili kujua namna ilivyotokea hapo hutumia rejesta yao kwanza ndipo huanza kufafanua kwa wahusika. Katika sababu hii, 3 (20%) ya wahojiwa ndio walipendekeza kuwa rejesta hutumika panapokuwepo na shughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani kama vile ajali inayohusisha magari.

### 4.5.2 Mjadala wa Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari wa Usalama Barabarani

Katika swali hili, dodoso liligawiwa kwa askari wa usalama barabarani 15. Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ya askari wa usalama barabarani, wahojiwa hao walikuwa na majibu ambayo yamebainishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 4.13: Data zaidi za Sababu za Ukuaji wa Rejesta ya Askari wa Usalama Barabarani**

| Mjadala wa sababu za ukuaji wa rejesta ya askari polisi | Idadi | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Matumizi ya kila siku | 2 | 14 |
| Uwepo wa matukio ya uvunjanji wa sheria za usalama barabarani | 8 | 53 |
| Uwepo wa shughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani kama vile ajali inayohusisha magari | 5 | 33 |
| **Jumla** | **15** | **100** |

Chanzo: Data za Utafiti (2017)

Kutokana na takwimu zilizopo katika Jedwali 4.13 zilizopatikana uwandani, motokeo ya utafiti yalionyesha kuwa watoa habari 8 (53%) walithibitisha kuwa uwepo wa matukio ya uvunjaji wa sheria za usalama barabarani ni sababu mojawapo inayopelekea askari wa usalama barabarani kutumia rejesta, pia 5 (33%) walisema kuwa uwepo wa shughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani kama vile ajali inayohusisha vyombo vya moto ni sababu mojawapo inayopelekea askari wa usalama barabarani kutumia rejesta. Watoa habari 2(14%) walisema kuwa rejesta hutumika kwa matumizi ya kila siku na hii imepelekea askari wa usalama barabarani kutumia rejesta kurahisisha mazungumzo wawapo kazini.

Hivyo, kutokana na data zilizopatikana katika lengo la tatu, zimeonesha kufanana na utafiti wa Mwansoko (keshatajwa) ambaye alichunguza rejessta ya vyombo vya usafiri, ambapo imeonesha kuwa sababu ya ukuaji wa rejesta ya vyombo vya usafiri haitofautiani na sababu ya ukuaji wa rejesta ya askari polisi.

## 4.6 Hitimisho La Jumla

Sura ya nne, imeonesha matokeo ya malengo yote matatu ya utafiti ambapo kiwango cha utumiaji wa rejesta ya mazungumzo ya askari polisi kimebainishwa, kazi za rejesta ya askari polisi zimeelezwa na pia sababu za ukuaji wa rejesta za askari polisi zimejadiliwa.

# SURA YA TANO

# MATOKEO YA UTAFITI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imegawanywa katika sehemu sita. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi wa sura yenyewe, sehemu ya pili inahusu muhtasari wa utafiti, sehemu ya tatu inaeleza matokeo ya utafiti, sehemu ya nne inaeleza mchango wa utafiti, sehemu ya tano inahusu mapendekezo mbalimbali na sehemu ya sita inaeleza maeneo yanayohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

## 5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu, ulilenga kuchunguza rejesta ya mazungumzo ya askari polisi katika lugha ya Kiswahili jijini Mbeya.Utafiti ulijikita kuchunguza mambo makuu matatu. Mosi, kubainisha kiwango cha rmatumizi ya rejesta askari polisi zinavyozungumzwa, pili kueleza kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi, tatu kujadili sababu za ukuaji wa rejesta ya askari polisi.

Nadharia ya rejesta ilitumika kuonyesha namna lugha ilivyotumika kulingana na muktadha maalumu. Kupitia nadharia hii imebainika namna lugha ilivyotumika katika muktadha wa mazungumzo ya askari polisi wawapo kazini kama ilivyochambuliwa katika sura ya nne.

Utafiti huu ulifanyika jijini Mbeya katika vituo vya kazi vya askari polisi ambavyo ni kituo cha polisi cha kati na kituo cha usalama wa barabarani, kwa sababu ndiyo maeneo makuu yanayopokea na kushughulikia taarifa mbalimbali kuhusiana na usalama wa raia na mali zao taarifa kuhusu usalama wa madereva na vyombo vya

usafiri. Jumla ya watoa taarifa 30, askari polisi na askari wa usalama barabarani walisaidia kupata data ambazo zimetumika katika utafiti huu. Utafiti huu ulitumia mbinu za ushuhudiaji, mahojianona dodoso katika mchakato wa kukusanya data.

Hivyo, kutokana na takwimu zilizopatikana uwandani, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kiwango cha utumiaji wa rejesta ya mazungumzo ya askari polisi ni kikubwa. Kwa mfano imeonekana kuwa neno Lindo ni miongoni mwa maneno rejesta yanayotumika katika jeshi la polisi, neno afande hutumika mara nyingi zaidi katika mazungumzo ya askari polisi,pia neno mlalamikaji hutumiwa katika rekodi za askari, vilevile watoa habari walisema kuwa neno mshitakiwa hutumika katika kazi ya askari polisi. Pamoja na data hizo ilithibitika kuwa neno mtuhumiwa linatumika katika kazi ya askari polisi.

Pia, watoa habari walibainisha kuwa neno vunja linatumika wakati raia wanapofika kutoa taarifa juu ya tukio la kihalifu lililotokea, pia wahojiwa walisema kuwa neno unyanyasaji linatumika mara kwa mara pale ambapo askari polisi wanapopewa taarifa za unyanyasaji wa matukio mbalimbali na hata neno Leseni linatumika katika lugha hiyo wakati madereva wanapofika kushughulikia leseni zao zinazowatambulisha kuwa wamepitia mafunzo ya kuendesha vyombo vya moto.

Vilevile katika lengo la pili la utafiti huu, watojia habari (askari polisi na askari usalama barabarani) walikuwa na maoni tofauti katika kuelezea kazi ya rejesta katika mawasiliano ya askari polisi. Kutokana na takwimu zilizopo, matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa watoa habari walithibitisha kuwa rejesta hutumika kuficha usiri, kupunguza idadi ya maneno, kurahisisha mazungumzo wawapo kazini, kupamba

lugha, kurahisisha mawasiliano, na kumtambulisha mzungumzaji katika kutofautisha ngazi ya kazi.

Pia katika lengo la tatu, matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa sababu zinazopelekea ukuaji wa rejesta ni kutunza taarifa ili zisivuje kwa mtu mwingine kabla upelelezi haujakamilika. Hivyo askari wa upelelezi anapokuwa katika shughuli hiyo kuna wakati hulazimika kutumia rejesta yao mara anapowasiliana na mkuu wake wa kazi ambaye alimwagiza kufanya kazi husika. Vilevile mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa kitengo cha mawasilino askari huyo alieleza kuwa sababu inayopelekea ukuaji ya rejesta hii ni kumficha adui, hasa askari polisi wanapokuwa mitaani kushughulikia tukio la uvamizi fulani unaohusisha matumizi ya silaha kati yao na wahalifu, askari huwasiliana kwa rejesta ili adui asitambue maelekezo waliyopewa.

Askari polisi wa usalama barabarani hutumia rejesta kwa sababu ya uwepo wa matukio ya uvunjanji wa sheria za usalama barabarani. Hii ilithibitika kuwa pale inapotokea dereva amevunja sheria labda amesababisha ajali, askari husika anapotoa taarifa kwa mkuu wake wa kazi kwa kutumia redio call hutumia rejesta yao.

Aidha mtafiti alifanya mahojiano na askari polisi wa usalama barabarani katika pointi nyingine ya ulinzi, yeye alieza kuwa sababu inayopelekea ukuaji wa rejesta ya askari poilisi niuwepo wa shughuli mbalimbali zinazofanyika wanapokuwa katika mchakato wa kulinda usalama wa barabarani kama vile ajali inayohusisha magari tu inapotokea askari huitwa na wanapima ili kujua namna ilivyotokea hapo hutumia rejesta yao kwanza ndipo huanza kufafanua kwa wahusika.

## 5.3 Mapendekezo

(i) Askari polisi na askari usalama barabarani waendelee kutumia rejesta katika kazi zao ili kuboresha utendaji wa kazi na kuficha usiri

(ii) Serikali na washikadau wengine waendelee kutoa mafunzo mbalimbali kwa askari polisi na askari usalama barabarani ili rejesta itumike kwa ufanisi zaidi.

(iii) Utawala wa jeshi la polisi uendelee kufanya utafiti na kuibua rejesta zingine zaidi ili kuboresha utendaji kazi.

## 5.4 Mapendekezo Kwa Tafiti Fuatishi

Utafiti huu umedokeza maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa utafiti zaidi ambayo ni haya yafuatayo:

(i) Utafiti zaidi ufanywe kuhusu athari za rejesta ya askari polisi katika kukikuza aa kudumaza lugha ya Kiswahili

(ii) Pia utafiti unaweza kufanywa zaidi kuiangalia rejesta katika vipengele vya semantiki na pragmatiki

## 5.5 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imejadili juu yamuhtasari, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo kwa tafiti fuatishi na kisha umeonesha maeneo mengineambayo yanaweza kufanyiwa utafiti zaidi na watafiti wengine katika taaluma za isimu, isimujamii na fasihi ambazo bado zinahitaji tafiti zaidi.

**MAREJEO**

Adamu, J., na Kamuzora, F. (2006). *Research methods for Business and Social Studies*.Morogoro: Mzumbe Book Project.

Bell, A. (1984). “Language Style as Audience Design” *Language in Society, 13(2),* 145-204.

Biber, D., (1988). *Variation Across Speech and Writing.* Cambrige: Cambrige University Press Buliba, A., Kiman, N., na Alice, M. (2006).*“Isimu Jamii kwa wanafunziwa Kiswahili,* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Burns, T., (1957). *First Study of Middle Management Work in the Work of Managers; Towards a Practise Theory of Management*: Oxford: Oxford Universirt Press.

Cruse, A., (2004). *Meaning in Language; An Introduction to Semantics and Pragmatic*. Nairobi: Oxford University Press.

Enon, J. C. (1998). *Educational Research, Statistics and Measurements*. Kampala: Makerere University Press.

Ghadessy, M., and Halliday, M. A. K. (1988). *Registers of Written English.* London: Printer Publishers Limited.

Habwe, J. na Karanja, P. (2007). *Missing ya Sarufi ya Kiswahili Nairobi*: Phoenix Publishers.

Halliday, M. A. K. (1989). *Spoken & Written Languages*, London: Oxford University Press.

Hamisi, A., na John, G. K. (2002). *Uchunguzi wa Sarufi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Hymes, D. (1964). *Language in Culture and Society.* New York: Harper & Row.

Hymes, D. (1996). *Ethnography, Linguistic, Narrative Inequality: Towards an Understanding of Voice*. Bristol P.A: Taylor and Francis.

Jung, K. (2008). "World Cup Football Live on Spanish and Argentine Television: The Spectacle of Language" Katika Lavric, Eva, Pisek, Gerhard, Skinner, Andrew, Stdler na Wolfgang (Wah), The Linguistic of Football, Tubingen: Gunter Narr, 343 -358.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu Jamii*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kombo, D. K., and Trompo, D. L. (2006*) Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology Methods and Techniques*.New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Labov, W., na Trudgill, P. (1966). *The Basic Variation Theorists.* New York: Cambridge University Press.

Leckie-Tarry, H., (1995). Language & Context: A Functional Linguistics Theory of Register. London: Printer Publishers.

Massamba, D. P. B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.*Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mathokoo, P.M., (2007). *Isimu Jamii: Misjngi na Nadharia*. Nairobi: Njiguna Books.

Mdee, S. J. (1980). *Kiswahili na Matumizi yake*. Nairobi: Intercontinental Publishers.

Mdee, S. J. (1980). Kiswahili na Matumizi yake, Nairobi: Intercontinental Publishers.

Mdee, S. J. (2014). *OSW 613: Isimu Jamii*.Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimu Jamii, Nadharia ya muktadha wa Kiswahili*.Osaka: University of Foreign Studies.

Metin, T. (2010). "Different Language Styles in News Papers: An Investigative Frame work", *Journal of Language and Linguistic Studies, 6(2),* 104 – 126.

Mgullu, R. S. (1999) *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*, Nairobi Kenya.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*, Nairobi: Longhorn Publishers.

Mhango, P., (2013). "Tasinifu Matumizi ya Lugha ya Kiswahili na Utambulisho wa Wafanyakazi wa Mgodi wa Buzwagi". Kahama Tanzania: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Msanjila na Wenzake., (2010). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu Jamii*.Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., na Massamba, D. P. B. (2010). *Isimu Jamii Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

Mwansoko, H. J. M. (1998). *Simo na Nafsi yake katika Kiswahili katika kioo cha Lugha.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Ngole, C. (2013). "Lugha Inayotumika katika Masoko ya Nguo za Mitumba. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Polit, D. F., Hungler, B. P. (1999). *Nursing Research: Principles and Methods (6$^{th}$ edn)* Philadelphia: J.B Lippincon.

Romaine, S., (1994). *Language in Society: An Introduction to Socialinguistics.* Oxford: Oxford University Press.

Suriano, M., (2007 “Mimi ni msanii; kioo cha jamii. Urban Youth Culture in Tanzania as seen- Through Bongo Fleva and Hip- Hop. *Swahili Forum 14(3)*, 207 -223.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wikipedia http google Mganga wa kienyeji, (1988). Makala ni elimu kuhusu magonjwa wa watu mwilini na rohoni, jinsi ya kuzuia magonjwa na kuhusu njia ya kurudisha uzima: Imepakuliwa Tarehe 2/5/2016 kutoka: https://sw.wikipedia.org/wiki/TibaPeru.

Young, S. (2010). *Cross – Lingua Spoken Languge Understanding for Unaligned Data using Disriminative Classfication Models and Machine Translation*. Tokyo: Interspeech Publishers.

# KIAMBATANISHO

## Kiambatanisho A: Dodoso la Utafiti Kuhusu Rejesta Katika Vituo vya Kazi vya Askari Poilisi Jijini Mbeya

1. Jina……………………………………………………..……………………..
2. Kituo Unachofanyia Kazi………………………………………………………….

   Weka Alama Ya Tiki [ ] Mahali Sahihi
3. Jinsia Yako Ni Me [ ] Ke [ ]
4. Umri Kijana [ ] Mtu Mzima [ ]

Jibu maswali yafuatayo kama utakavyoelekezwa:

1.Je ni kwa namna gani rejesta ya askari polisi huzungumzwa? Andika maneno yafuatayo kwa rejesta ya askari polisi

(i) Afande ………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………….

(ii) Lindo……………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………….

(iii) Mlalamikaji …………………………………………………………………..

………………………………………………………………………….

(iv)Mshitakiwa……………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………...

(v)Shahidi…………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………

(vi)Kituoni……………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………

(vii) Haraka……………………………………………………………………..

……………………………………………………………………..

viii) Nimekusoma…………………………………………………………..

………………………………………………………………….

(ix) Nitatekeleza………………………………………………………….

……………………………………………………………………..

**(x)** Sheria……………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

(xi) Barabara……………………………………………………………………….

……………………………………………………………

(xii) Ndiyo…………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………..

(xiii)

Polisi…………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………….

(xiv) Mkamateni……………………………………………………………………

……………………………………………………………………………

(xv)Kesi…………………………………………………………………………….

………………………………………………………………………………….

(xvi)Vunja…………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………….

(xviii)Unyanyasaji…………………………………………………………………

………………………………………………………………………………….

(xix)Jinai…………………………………………………………...………………

(xx)Dereva…………… …….……………………………………………………….

.........................................................................................................................

2. **Sehemu ya tatu: (**Je ni nini kazi ya rejesta katika mazungumzo ya askari polisi wa jiji la Mbeya? Weka alama (N) kuthibitisha na alama (H) kukanusha

(i) Je, rejesta hutumika kuficha siri?

(a) ndiyo [ ]

(b) hapana [ ]

Toa mfano,

Kuna mtu nimempa ***kihusika chako*** (namba ya simu)

(ii)Je, r ejesta hutumika katika kupunguza I dadi ya maneno

(a) ndiyo [ ]

(b) hapana [ ]

Toa mfano,

***Njoo Chalii IM*** (njoo kituo cha polisi cha kati haraka sana)

(iii)Rejesta hutumika kurahisisha mazungumzo

(a) ndiyo [ ]

(b) hapana [ ]

Toa mfano,

Naelekea ***Hotel*****Mike (H & M)(** naelekea nyumbani)

(iv)Je, rejesta ni kitambulisho cha mzungumzaji?

(a) ndiyo [ ]

(b) hapana [ ]

Toa mfano,

**Chui 1**: Control ***kwa Kanga 1…”,*** (chui moja ni mkuu wa poilsi wa eneo husika kamanda wa polisi)

**Control**: ***Nakupata kanga 1…”***

**Chui 1**: ***Niitie kanga4….”***

(v) Hutumika kupamba lugha

(a) ndiyo [ ]

( b) hapana [ ]

Toa mfano,

Nimekusoma ***5/5*** (***nimekuelewa kwa usahihi***)

(vi) Hutumika kuokoa muda?

(a) ndiyo [ ]

( b) hapana [ ]

Toa mfano,

Vipi afande kuna mafanikio? ***NIL*** (ina maana hakuna kitu walichopata katika upekuzi wao)

**Sehemu ya nne**: Ni sababu zipi zinaopelekea ukuaji wa rejesta katika mawasiliano ya askari polisi?

(i)……………………………………………

(ii)…………………………………………. ..

(iii)…………………………………………..

(iv)…………………………………………..

(v)…………………………………………...

**Kiambatanisho B: Msamiati Uliokusanywa**

| Na | Msamiati | Maana yake katika rejesta ya askari Polisi |
|---|---|---|
| 1 | Afande | Alfa Fox Alfa November Delta Echo |
| 2 | Lindo | Lima India November Delta Osca |
| 3 | Mlalamikaji | Mike Lima Alfa Lima Alfa Mike India Kilo Alfa Juliety Idia |
| 4 | Mshitakiwa | Mike Siela Hotel India Tango Alfa Kilo India Wisky Alfa |
| 5 | Shahidi | Siela Hotel Alfa Hotel India Delta India |
| 6 | Kituoni | Kilo India Tango Uniform Osca November India |
| 7 | Haraka | Hotel Alfa Romeo Alfa Kilo Alfa |
| 8 | Nimekusoma | November India Mike Kilo Echo Kilo Uniform Siela Osca Mike Alfa |
| 9 | Nitatekeleza | November India Tango Alfa Tango Echo Kilo Echo Lima Echo Zulu Alfa |
| 10 | Sheria | Siela Hotel Echo Romeo India Alfa |
| 11 | Barabara | Bravo Alfa Romeo Alfa Bravo Alfa Romeo Alfa |
| 12 | Ndiyo | November Delta India Yankee Osca |
| 13 | Polisi | Papa Osca Lima India Siela India |
| 14 | Mkamateni | Mike Kilo Alfa Mike Alfa Tango Echo November India |
| 15 | Kesi | Kilo Echo Siela India |
| 16 | Vunja | Victa Uniform November Juliety Alfa |
| 17 | Unyanyasaji | Uniform November Yankee Alfa November Yankeee Alfa Siela Alfa Juliety India |
| 18 | Leseni | Lima Echo Siera |
| 19 | Jinai | Juliety India November Alfa India |
| 20 | Dereva | Delta Echo Romeo Echo Victa Alfa |